UTAMBULISHO

. . .tunapolisoma Neno. Tukikumbuka, baada ya ibada hii alasiri hii, labda mtarudi makanisani mwenu, kwa ibada ya usiku. Nitajaribu kuwaachia mapema ili muweze kufanya hivyo.

2 Sikilizeni. Kama ningalikuwa katika mji huu, mumu humu, ningehudhuria kwenye haya-haya makanisa hapa. Hakika ningehudhuria. Silisemi hilo. . .Kamwe sikuambiwa niseme hili. Kuna watu walio wazuri, ndugu halisi. Na kisha kila mmoja wenu ambaye alimkubali Kristo, kama hawakupata jina lako, kwa nini usiwatafute, kwa ajili ya ubatizo wa Kikristo, na uwaruhusu wakuongoze hadi kwenye ubatizo wa Roho Mtakatifu.

3 Kama huna kanisa, inakubidi, unaona; utakufa, kiroho, utafifia tu kabisa. Na kama huna kanisa, mbona usiende na kuzungumza nao, wangefurahi kukusaidia. Hao ni—hao ni—hao ni ndugu katika Kristo, na, hao, wangefurahi kukusaidia. Hilo si ni kweli, ndugu? [Wahudumu wanasema, "Kweli."—Mh.] Watafurahi sana tu kuwasadia, na kuwasaidia kuendelea, wafanye lolote ambalo wanaweza kwa ajili yenu. Mtu mwema, mwaminifu, mtu atakayechunga nafsi yako na kukutunza. Fanya hivyo.

4 Na kama ulimkubali Kristo, nao hawakupata jina lako, ulikuwa tu mahali fulani kwenye kiti ukamkubali, mbona usiende kuzungumza nao kuhusu ubatizo sasa, na ubatizo wa Roho Mtakatifu. Fanya hivyo sasa. Mungu awabariki.

5 Tunataka kusoma, alasiri hii, kutoka kwenye kitabu cha Wafilipi, mlango wa 2 wa Wafilipi. Nami nataka kuanza na kifungu cha 5.

Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu, ambayo ilikuwamo pia ndani ya Kristo Yesu:

Ambaye yeye mwanzo alikuwa yuna namna ya Mungu, naye hakuona kule kuwa sawa na Mungu kuwa ni kitu cha kushikamana nacho;

Bali alijifanya kuwa hana utukufu, akatwaa namna ya mtumwa, akawa ana mfano wa mwanadamu:

Tena alipoonekana ana umbo kama mwanadamu, alijinyenyekeza akawa mtii hata mauti, naam mauti ya msalaba.

Kwa hiyo tena Mungu alimwadhimisha mno, akamkirimia jina lile lipitalo kila jina:

Ili kwa jina la Yesu kila goti lipigwe, la vitu ambavyo ni vya mbinguni, na vya duniani, . . .vitu vilivyoko chini ya nchi:

Na kila ulimi ukiri ya kuwa Yesu ni Kristo yule Bwana, kwa utukufu wa Mungu Baba yetu.

Na tuinamishe vichwa vyetu kwa muda kidogo.

6 Bwana wetu, tunakukaribia Wewe sasa katika Jina takatifu ambalo-ambalo lina Jina la Mbinguni, na familia yote duniani imeitwa kwalo. Naye alitwambia, alipokuwa hapa, "Mkimwomba Baba neno lolote kwa Jina Langu, nitawapeni." Tu watu rahisi tu, Bwana, bali tunaamini hilo kuwa ni kweli. Tunaamini kwamba tuliombalo twalipokea, kwa sababu kama ninii zetu—kama nafsi zetu hazituhukumu, kama hatuna hisia zozote mbaya za yale tumetenda, ambayo ni makosa, basi tuna hili hakikisho kwamba Mungu atatusikia. Kwa hiyo tunaomba rehema, alasiri hii, kwa ajili yetu sote.

7 Na sasa naomba kwamba Wewe utawajalia wasikilizaji hawa wanaongoja, sasa, uponyaji kwa kila mtu ambaye yupo katika Uwepo wa Mungu. Jalia hii iwe mojawapo ya ibada kuu sana za uponyaji ambazo tumewahi kuwa nazo. Jalia jambo fulani litukie, Bwana. Sisi hatujui jinsi gani lingetukia, au jambo gani jingine lingeweza kutendwa, bali tunaomba kwamba Roho Mtakatifu atakuwa na utangulizi alasiri hii, kuingia ndani ya kila moyo na kila akili. Kama vile tulivyosoma sasa hivi, "Iweni na nia ile ile iliyokuwa ndani ya Kristo ndani yenu." Naomba, Mungu, ya kuwa kama tunavyoona kwamba akili ni mnara wa kuongoza utu wote, kwamba inatuongoza sisi, na jalia nia ile iliyokuwa ndani ya Kristo iwe ndani yetu alasiri hii. Na Yeye sikuzote alikuwa anaamini Neno. Na sasa jalia kuwe na mmimino mkuu wa Uwepo Wake juu yetu.

8 Nami naomba kwa ajili ya hawa wahudumu, Bwana, ambao wameshirikiana katika mkutano huu, kwamba kila moja ya makanisa yao yatanufaika kwa manufaa makuu sana ya kiroho na ya mali, kwa sababu ya msimamo wao, kujaribu kuileta kwa watu wao, ile Injili, kwa kila mtindo wa kweli ambao wanajua inahubiriwa kwake. Nami naomba, Baba, kwamba Wewe utawabariki. Na hebu watu wawathamini, wakijua kwamba—kwamba wanatenda hilo kwa ajili yao na kwa ajili ya Injili; kwamba hebu nao, kwa shukrani, wasaidie na kufanya juhudi, na kuendeleza Kusudi ambalo tunajaribu kulileta duniani, Bwana Yesu.

9 Sasa, Baba, tunaomba kwamba Wewe utachukua hayo Maneno kama tulivyoyasoma, na Wewe Ndiwe Unayejifasiria, kwa hiyo tunaomba kwamba Wewe utafasiri Hilo katika mioyo yetu leo. Na wakati tunapoondoka, leo, jalia tuseme kama wale waliotoka Emau, "Je mioyo yetu haikuwaka ndani yetu Yeye alipozungumza nasi tulipokuwa njiani?"

10 Wabariki, Mungu, wote hawa watoto wachanga waliozaliwa upya waliokuja Kwako sasa hivi. Naomba, kwa njia yao ya uchanga, kwamba watalishwa na maziwa ya Injili

yasiyoghoshiwa, kwamba watakua katika kimo kikuu cha Kristo, kwamba waweze kuwa wanenaji na watumishi Wake, kumtumikia Yeye katika wakati huu mkuu wenye uvuli ambao tunaishi ndani yake, katika Nuru za jioni. Tupatie hilo, Baba. Tunaomba hili katika Jina la Yesu. Amina.

Mwaweza kuketi.

11 [Dada ananena kwa lugha. Sehemu tupu kwenye kanda. Ndugu mmoja anatoa tafsiri—Mh.] Amina. Amina. Nafikiri ujumbe huo ungekuwa wa kuwafariji watakatifu, na wa kutukuza. . . kuwashauri waongofu wachanga wamkaribie Mungu na kuendelea katika Imani. Mungu ashukuriwe.

12 Sasa nataka kuchukua somo hili kwa muda kidogo. Inatupasa, hatutaweza kunena bali kwa muda kidogo tu, kwa sababu tumetoa karibu kadi mia tano za maombi, na wote yapasa waombewe.

13 Kwa hiyo sasa natenda hili ili kwamba liweze kusaidia. Sijui kama sauti yangu haitoi mwangwi. Mwaweza kunisikia kule nyuma kabisa, vema? Inasikika kwangu kama inarudi nyuma hapa. Na usiku uliopita, katika kufanya wito wa madhabahuni, niliwaza kwamba hiyo huenda ndio sababu watu wasingeweza kuelewa, kwamba ilikuwa na mwangwi.

14 Sasa nataka kuchukua somo hili alasiri hii: *Utambulisho*.

15 Sasa, mtu yeyote, ambaye hana budi, tunaishi katika siku ambayo utambulisho unatakiwa. Huwezi, isipokuwa unajulikana kwenye benki, huwezi kulipwa hundi yako isipokuwa uwe na kitu fulani cha kujitambulisha.

16 Najua, mke wangu hawezi kulipwa hundi. Hata hivyo, tunapopata hundi yetu, tunaiweka katika benki. Bali halipwi hiyo, kwa sababu yeye haendeshi gari, hana namba ya mfanyakazi au chochote cha kujitambulisha. Hivyo basi ni vigumu kwake kulipwa hundi. Yakupasa uwe na kitambulisho rasmi, nami nafikiri ni wakati tu ambao tunaishi.

17 Kama ukiangalia, kama ukienda kwenye kanisa fulani la kimadhehebu, kama la Kimethodisti, Kipresbiteri, Kiluteri, au lolote lile, yakupasa uwe na kitu fulani cha kujitambulisha kama utakwenda kunena. Yakupasa uwe na cheti, au kadi, au kadi ya ushirika, au kitu fulani cha kujitambulisha wapate kujua mahali unakotoka na yale utakayosema jukwaani. Yapasa utambulike. Na—na ni wakati wa kutambulika.

18 Sasa yote yale ambayo hutukia katika mazingira ya kawaida ni mfano tu wa kinachoendelea katika mazingira ya kiroho. Sisi pia, Kanisa la Kikristo Lenyewe, ambalo si la kimadhehebu, bali la Asili. Ni Mwili wa kisiri wa Kristo, na Huo unatambulika, pia. Una vitambulisho. Yesu alijitambulisha.

19 Na sasa tutazungumza alasiri hii juu ya vitambulisho, katika sura ya Biblia. Tunaenda ku, au kutambulisha hali yetu ya sasa, na wahusika wa Biblia, wa nyakati zingine.

20 Sasa, twashangaa wakati mwingine jinsi—jinsi tungeonekana kama tungejaribu kuangalia katika kioo na kuona jinsi tunavyoonekana. Yanikumbusha hadithi ndogo niliyoisikia wakati mmoja, ya familia moja iliyoishi huko Kentucky mashambani, mahali ninakotoka, nyuma kule katika nchi ya milima mahali ambako kuna . . .

21 Vema, nyanya yangu aliishi kufikia umri wa miaka mia moja na kumi, naye hakuona ila gari moja, na kulileta kutoka kwenye mteremko wa kale, kufikia mahali ambapo nilileta langu, ilichukua karibu saa nane kwenda mwendo wa yapata maili nne; tukiweka magogo katika hori, na kadhalika, ili kulivusha. Yeye kamwe hajaona ga—ga—garimoshi, au chochote cha kale vya kutosha. Wakati alipokufa, miaka mingi iliyopita, alikumbuka kuuawa kwa rais Lincoln, naye aliishi kufikia umri wa miaka mia moja na kumi.

22 Nami nadhani yeye kamwe hajawahi kuwa na jozi tatu au nne za viatu, maishani mwake mwote. Nami naweza tu kuona zile njia ndogo za kale sasa, kama njia ya mnyama mdogo wa mwituni ikielekea kwenye chemchemi, ikiwa ni alfajiri kabla ya mapambazuko; akiwa na ndoo kubwa ya mwelezi, yenye mikono, ina mikono ya shaba, akienda kuteka maji, aje kupika. Kakaa amenyoosha miguu yake maskini, mbele ya jiko la kale, namna hiyo, nyufa kubwa, nazo zinatoa damu.

23 Bali wakati alipokufa, alinikumbatia kwa mikono yake, nilimshika mikononi mwangu na kulia, nikimwombea namna hii. Maneno ya mwisho niliyomsikia akisema, yalikuwa, "Mungu abariki nafsi yako ndogo sasa na daima." Nilikuwa mvulana tu wakati huo. Bali alimjua Kristo kama Mwokozi wake, bali hawakuwa na vitu vingi sana vya ulimwengu huu.

24 Basi kutoka kwenye hadithi hii laja hili, kwamba watu hawa wasingeweza kugharimia kioo cha kujiangalia. Hawakuwa nacho, na baba alikuwa tu na kipande cha—cha kioo alichokuwa amekishikiza kwenye mti, kwa ajili ya kunyoa, kule nje. Walikuwa na mvulana mdogo, naye angeninii . . . hiki kipande kidogo cha kioo, mbona, hakuwa amewahi ku—kufikia mahali kilipokuwa, ajione mwenyewe. Kwa hiyo alikuja kutembea mjini kwa mmoja wa dada za mama yake aliyekuwa ameolewa na—na mwanaume aliyekuwa amekuja Indiana, na basi waliishi nje huko. Basi walikuwa na nyumba, wote wangeninii . . .

25 Nyumba ya mtindo wa kale, ilikuwa, walikuwa na kioo kikubwa mlangoni, wakati mwingine, wakati angalikwenda kwenye—kwenye—kwenye vyumba vya kulala. Sijui kama mmoja wenu anakumbuka hiyo milango ya kale, au hapana,

ambayo ilikuwa na kioo cha urefu kamili toka juu hadi chini ya mlango.

26 Kwa hiyo huyo mvulana mdogo, alifika kwenye nyumba ya shangazi yake, naye alikuwa akikimbia hapa na pale kama ambavyo mvulana yeyote mdogo angefanya, na—na wao walimwangalia. Ndipo a—alianza ku—kupanda vipandio. Na, alipofanya hivyo, pale kwenye mwisho wa vipandio, wakati alipokuwa anakaribia mwisho wa vipandio, alianza kuona mvulana mwingine mdogo akitokea. Ndipo alisimama na kumtazama yule mvulana mdogo. Naam, ilikuwa... Yeye alimpungia mkono, naye akarudishia kumpungia. Naye akaendelea kusogea karibu zaidi na zaidi, akimwangalia yule jamaa mdogo. Jambo la kwanza, alinyoosha mkono wake. Akatazama huku na kule. Wazazi wake walikuwa wakimwangalia, maana alikuwa hajawahi kuona kioo awali. Akasema, "Vema, huyo ni mimi."

27 Basi najiuliza tu, leo, kama tusingaliweza kuangalia ndani ya Biblia, na kusema, "Huyo ni mimi," tunapojiuliza huyo ni nani, ni mtu gani kwenye Biblia tunayefanana naye. Na hebu tuchukue tu hilo kwa ajili ya somo fupi tu sasa na tukae nalo kwa muda kidogo. Na tunapotazama kwenye Neno la Mungu, hebu na tujitambulishe wenyewe, kwa maana Yeye alitoa wengine humo kuwa mifano ya kile tulicho. Sasa kumbuka kwamba Mungu huchukua Roho Wake...au huchukua mtu Wake, bali kamwe si Roho Wake; Shetani huchukua mtu wake, bali kamwe si pepo wake. Kwa hiyo hebu na tuone kama tunaweza kujitambulisha hali yetu ya sasa na watu wa Biblia. Sasa, hao, Biblia ilisema, "Mambo yote hayo yalitukia, katika siku hizo za nyuma, kuwa mifano kwa ajili yetu." Mambo hayo ni mifano kwa ajili yetu.

28 Tabia yetu huumba sura ya kile tulicho, tabia yetu ya uhai ulio ndani yetu.

29 Sasa hebu chukua seli zazi ndogo ya uhai, na iwapo kama ni—kama ni seli zazi ya ninii—ya ndege, itazaa ndege. Na kama ni seli zazi ya—ya ngano itazaa ngano. Seli zazi ya mahindi, itazaa mahindi. Unaona, uhai ulio ndani yake huumba tabia yake.

30 Ndipo tunaona jambo lile lile, kama ulivyo uhai wa kansa. Unaona, seli zazi, seli zazi ya uhai wa kansa, huumba kansa. Ni uhai mwovu. Uhai wa uvimbe ungeumba uvimbe, na kadhalika.

31 Unaona, sisi, tabia zetu zinaumbika kutokana na kile kilicho ndani yetu, na hali yetu ya nje huonyesha tu yale yaliyo ndani. Kile tulicho, jinsi tunavyoenenda, haidhuru tunasema nini, maisha yetu hunena kwa sauti kubwa zaidi kuliko maneno yetu.

Kama tungalisema, "Mimi ninamwamini Mungu."

Nami ningesema, "Vema, Je! unaamini Biblia yote?"

32 "Vema, sijui." Basi, unaona, midomo yako—yako—yako, ninii yako hasa . . . maisha yako basi yananena kwa sauti kubwa zaidi kuliko vile maneno yako yangekuwa yakinena.

33 Kama ukisema, "Mimi ni Mkristo. Siamini katika kutenda . . . nami naamini yote aliyosema Mungu ni Kweli." Kisha uishi maisha ya aina yoyote baada ya hapo? Unaona, maisha yako—yako hunena kwa sauti kubwa zaidi kuliko yale ushuhuda wako unavyonena.

34 Na, unajua, hicho ni mojawapo ya kikwazo kikubwa sana ambacho kanisa la Mungu likonacho. Muuza pombe haramu, mcheza kamari, hao watu ni . . . sisi—sisi sote tunajua wanaelekea njia ipi, nao wanajua, wenyewe. Bali jamaa yule anayekiri kuwa Mkristo, mwanamke yule anayekiri kuwa Mkristo, na kisha anaishi kitu tofauti, ndicho kikwazo kikuu sana ambacho ulimwengu wa nje umepata, ambacho—ambacho—ambacho kiko katika ulimwengu wa nje, popote. Ni kibaya zaidi kuliko chochote ulimwengu unachoweza kutoa, ni mtu ambaye anapaswa kuwa Mkristo na kisha anaishi kitu fulani kingine tofauti. Kusema uongo, kuiba, kulaghai, na kutenda mambo ambayo hapaswi kuyatenda, hiyo ni fedheha kwa ushuhuda wake wakati mnapowachukua watu ambao hutenda mambo hayo huko. Na hao ni hao . . . tabia yetu inaumbika humo kwa uhai ulio ndani yetu.

35 Sasa tungesema, "Yesu alikuja kuokoa kile kilichopotea." Hilo ndilo Yeye alitenda. Na Sasa ilipasa kuwe na kitu fulani kumwokoa huyu aliyepotea, kwa hiyo ilipasa iwe ni mtu tofauti na huyu aliyepotea. Kwa hiyo tunaona basi, wakati Mungu alipotazama chini juu ya huu uumbaji Wake, ambao alikuwa ameufanya kwa ninii . . . Yake . . . tabia za hii dunia; tabia Yake ya upendo, Mwenyewe, iliumbika katika Utu wa Yesu Kristo, kuwa Mwokozi wa ulimwengu. Yeye . . . hili lilifanyika ili aweze kulipa adhabu ya kifo kwa ajili yetu, na atukomboe. Kwa hakika ilitimiza Yohana 3:16, unaona, kwamba "Mungu," hakuna mtu mwingine angaliweza kutenda hilo. Yesu asingeweza kuwa mtu mwingine yeyote. Hapakuwa na mtu mwingine popote ambaye angeweza kuleta Mtu kama Yesu Kristo, bali Mungu Mwenyewe.

36 Sasa hapakuwa na chochote Mbinguni, ambacho kingaliweza kutenda hilo. Unajua, Yohana alitazama ndani ya—ya Kitabu kule, Biblia, tunaona kwamba aliona hapakuwa na yeyote duniani aliyestahili kuchukua kile Kitabu, kile cha Ukombozi, wala hapakuwa na yeyote Mbinguni aliyestahili. Hapakuwa na yeyote chini ya dunia au popote, aliyeweza au aliyestahili kuchukua kile Kitabu, kufungua ile Mihuri, au hata kukitazama Hicho. Naye alilia kwa sababu ndani ya hiki Kitabu kulikuwamo na Kitabu cha Ukombozi, jina lake mwenyewe lilikuwa humo, na hapana yeyote aliyestahili.

37 Na kisha mmoja wa wale wazee akasema, “usiogope, kwa maana Simba wa Kabila la Yuda ameshinda, Naye amestahili.”

38 Basi Yohana alitazama ili aone Si—Simba, naye akaona ni Mwana-Kondoo na ni hapana budi aliona ni Mwana-kondoo aliyechinjwa. Alikuwa ni Mwana—Kondoo aliyelowa damu. Alisema alikuwa amejaa damu, kwa sababu, “Alikuwa ni Mwana—Kondoo aliyekuwa amechinjwa.” Na mwana-kondoo aliyechinjwa hulowa damu, bila shaka. “Na alikuwa amechinjwa tangu kuwekwa misingi ya ulimwengu. Yeye alikuja na kuchukua kile Kitabu.” Hapakuwa na mwingine yeyote angaliweza kukichukua.

39 Kwa sababu, kama ukipanda chochote kama vile gugu katika udongo. . . Yeyote wenu ninyi watu wa Arkansas anajua gugu ni nini. Na uweke hilo kwenye udongo, huwezi kutazamia kuvuna mazao ya mahindi kutoka kwa hilo. Hapana, hauwezi. Kwa hiyo kama ulichukua gugu na kuliweka pamoja na . . . na kulizalisha na gugu sumu, bado usingepata chochote. Unaona? Na, unaona, hakuna hulka ndani humo ila ambayo ingezaa hulka ile ile, uovu kwa uovu.

40 Kwa hiyo ilichukua kitu fulani ambacho sio kiovu, ambacho kingeweza kuumba tabia kama ya Yesu Kristo. Na ilikuwa ni Mungu akiangalia viumbe Vyake, na tabia Yake Mwenyewe ya upendo; akiona hao waliopotea, hata hivyo wakiwa katika sura Yake, walioumbwa kwa ajili ya utukufu Wake. Na, akiona hao waliopotea upendo Wake Mwenyewe ulimtoa Yesu Kristo. “Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe pekee.” Huyo alikuwa ni Mungu akijidhihirisha Mwenyewe, siyo mtu mwingine, bali Mwenyewe katika umbo la mwili, kuwakomboa waliokuwa wamepotea. Si ajabu ni lazima kwamba lilikuwa jambo la kusikitisha sana, wakati Mungu alipotazama duniani alighairi kwa kuwa amemfanya mwanadamu.

41 Wakati mmoja, mimi—nilikuwa nimemshika msichana wangu mdogo mkono, nasi tulikuwa huko Cincinnati, kwenye shamba la wanyama pori, nasi tulikuwa tunashuka tukitembea huko, tukitazama wanyama, nami nilisikia sauti kuu chini kule kwenye—kwenye—kwenye vizimba ambako wa—wanyama kama mbwa mwitu na chui milia, na kadhalika, walikuwa. Nilitembea chini huko. Na huko kulikuwa na kizimba kikubwa, kikubwa mno, loo, kirefu kama dari hili, labda. Nao walikuwa wamempata tu tai, kitambo kidogo, loo, majuma machache kabla ya hapo kutoka kwenye nini . . . na-kumuweka kifungoni. Sikuwa nimewahi kuona huzuni sana jinsi hiyo kwa ajili ya masikini jamaa huyo. Naye angerudi nyuma . . . Yeye ni ndege mkubwa, na yupo hapa amefungwa kabisa kizimbani na kitu fulani ambacho mwanadamu alikuwa amefanya, walikuwa wamemnasa katika kitu fulani, na kumuweka kizimbani.

42 Na ndege huyo mkubwa, alikuwa akivuja damu kichwani, upara wake mkubwa wa tai, hicho kichwa kikubwa cheupe; na—na mabawa yake, manyoya yote yalikuwa yamenyonyoka yakatoka namna hiyo. Na masikini ndege huyo mzee alikuwa amelalia mgongo wake; macho yake, machovu, yakitazama huku na kule. Yeye angeinuka, atembee kwenda upande mwingine wa kizimba, na kuangalia juu kuelekea mbinguni. Huko ndiko alikotoka.

43 Yeye ni ndege wa mbinguni. Hakuna chochote kinachoweza kumfuata. Mwewe angesambaratika, kujaribu kumfuata huyo. Hakuna chochote kinachoweza kumfuata huyo tai. Naye hupaa juu sana, macho yake yana ulinganifu na umbali wake wa kwenda juu, anaweza kuona anachofanya wakati akiwa juu kule. Kuna faida gani kwenda juu kule kama hujui unachofanya?

44 Kwa hiyo Mungu alilinganisha manabii Wake na tai, ambao hutangulia kuona mambo kabla hayajatukia.

45 Nami nilimwangalia akivuja damu, naye angelala kwa mgongo wake na kutazama juu namna *hiyo*. Makazi yake yako *huko* juu, bali mwanadamu alikuwa amemfungia kizimbani. Niliwaza, "Ni tamasha la kusikitisha jinsi gani!" Yeye angerudi nyuma, na angeruka, apigepige hizo mbawa zake kubwa na kupiga tu hizo nondo kwa kichwa chake, kisha anaanguka sakafuni tena. Alale hapo, mchovu, na akitazama pande zote namna *hiyo*; atazame mbinguni ambako alikuwa huru, juu huko, wakati mmoja, na sasa yumo kizimbani.

46 Nilisimama pale na kulia. Laiti wamgeliniuzia hicho kitu, ningelimfungulia. Kuona chochote kimefungiwa kwenye kizimba! Kama hilo lingemfanya mtu, anayependa pori, kama ninavyopenda pori, kama—kama hilo lingemfanya mtu alie, kwa kutazama hilo; na hilo lilikuwa tamasha la kusikitisha.

47 Bali, loo, hebu nikupe tamasha la kusikitisha zaidi, ni kuona wanaume na wanawake walioumbwa kwa sura ya Mungu, wapate kuchukua tabia Yake, hata hivyo wamefungiwa ndani ya vitu fulani, na wamefungwa ndani na mitego ya ulimwengu. Kumuona bibi kijana mrembo akishuka kuja mtaani, ni—ni—ninii halisi . . . yake—yake . . . mwanamke mrembo namna hiyo, na nywele zake nzuri zote zimekatwa; kuona uso wake una—una . . . uso mrembo, ulioumbika vizuri, umepakwa vipodozi vingi sana, huwezi kuelezea anafananaje. Anaonekana kama ameoza, kapaka rangi ya bluu chini ya macho yake, na—na macho kama mjusi, au mbwa mwitu, au kitu kama hicho. Na kumwona amevaa nguo ambazo yeye hata hapaswi kukamatwa nazo kwenye chu—chumba cha kulala mwenyewe, wakati milango imefungwa, akiwa amevaa hizo, na yuko nje mtaani akijianika mwenyewe namna hiyo. Na kuwaona wana wa Mungu, ambao wanapaswa kutambua kuwa huyo ni dada yao, wakiwa huko nje mtaani, wakimpigia miruzi na kujaribu

kumchukua, kumpeleka nje kwa malengo mabaya. Hilo ni tamasha la kusikitisha, kuona kwamba Shetani ameifungia kizimbani jamii ya binadamu.

48 Hakuna chochote kingaliweza kuokoa hiyo ila Tabia ambayo ingeweza kuja juu ya yote hayo. Hiyo, hiyo, hapakuwa na chochote ndani yake, na Hiyo ilipaswa kutoka kwenye Chemchemi safi ya Mwenyezi Mungu.

49 Huyo bibi mdogo mrembo, ambaye angeweza kuwa—kuwa malkia mdogo halisi, kwa maskini mhubiri aliyechoka, aingie na amchukue na kumweka mapajani mwake, na amkumbatie kwa mikono yake na—na kumtuliza, hakuna chochote kitakachochukua nafasi hiyo. Hiyo ni sehemu ya mwanaume. Hakuna mkono unaoweza kukugusa, wakati umechoka na kudhoofika, ila mke mkarimu, mpole hasa anayeelewa. Mwanaume anajua hilo.

50 Na kumwona nje namna hiyo, yuko ndani ya kizimba ambamo Hollywood imemfungia. Na—na mara nyingi hao wanawake wanadai kuwa ni Wakristo, na wanaimba kwenye kwaya, bali wamefungiwa kabisa kizimbani na pepo wasiyeweza kumwona. Hakuna haja ya wewe kujaribu kuwaonyesha hilo, kwao, inaonekana kana kwamba hali inaendelea kuwa mbaya zaidi na zaidi. Unaona? Hao hapo, Jezebel wa kisasa akitembea mitaani. Basi anasema "Nataka uelewe, mimi ni wa *hili*, nami. . ." Ona, hata hivyo, hicho-hicho kitu ambacho yuko ndani yake kime-kimemkatilia mbali kutoka kwenye chemchemi ya Uzima. Wakati alizaliwa awe malkia mdogo kwa mwanaume fulani, au mwanaume fulani ambaye alizaliwa mwa—mwa—mwana wa Mungu, na kuwazia yaliyowapata, loo, ni jambo la kutisha.

51 Basi, unaona, Mungu alishuka, na ile tabia ya Mungu alikuwa ni Kristo. Yeye, Yeye alikuwa sura ya Mungu. Alikuwa Mungu, aliyefanywa aonekane. Angalia, Mungu akifanyika aonekane.

52 "Hapo mwanzo alikuwa Mungu" Yeye hata hakuwa Mungu wakati huo. Hapana. *Mungu* ni "kitu cha kuabudiwa." Jambo pekee Yeye alikuwa, alikuwa Yule wa Umilele. Na ndani Yake kulikuwa na tabia, na hizo tabia zilikuwa ni mawazo. Na hayo mawazo yalinenwa yakawa maneno, nalo Neno likadhihirishwa.

53 Ni nini? Yote hayo ni Mungu, akifanyika kitu cha kugusika, na wewe ni sehemu ya Mungu. Na Yesu alikuja kukomboa wale waliowekwa kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana—Kondoo, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Ni jambo lililokuwa katika mawazo ya Mungu, na hao ndio Yeye alikuja kukomboa. Na hao, mara tu Hilo linapowagusa, wao wanaliona, kwa sababu ule Uzima uko humo ndani.

54 Bali kama huo Uzima haumo humo ndani, basi wanaweza kufanya nini? Unaona? Hawalioni Hilo. Kamwe hawataliona. Unaona?

55 Na jambo lote, kama Yesu alivyosema, "Siku ile, ninyi mtatambua ya kuwa Mimi ni ndani ya Baba, na Baba yuko ndani Yangu; Nami ndani yenu, nanyi ndani Yangu." Jambo hilo lote ni Mungu, akifanyika kitu. Kama vile mume na mke wakifanyika mmoja, pamoja, Mungu na Kanisa Lake wakifanyika Mmoja.

56 Sasa, ilichukua kitu fulani kumkomboa huyu mwanamke aliyeanguka, ambacho kilionyeshwa kwa kivuli katika Hawa, wakati alipoanguka. "Adamu hakudanganywa, bali mwanamke akidanganywa aliingia katika hali ya kukosa." Adamu alijua kwamba alikuwa anatenda kosa; mwanamke hakujua. Hiyo ndiyo sababu . . .

57 Siumizi hisia zenu, bali mnajua sikuzote ni jambo nililosimamia. Sikubaliani na jambo la wanawake wahudumu, kwa sababu haipaswi kuwa hivyo. Ona, yeye ni chombo kilicho dhaifu zaidi. Sasa tunaona kwamba huyo mwanamke alidanganywa na mtu mmoja akimnukulia Neno, na akalikosea kidogo tu, na hiyo ndiyo iliyosababisha shida yote; ndiyo sababu Paulo akasema, "Hebu na anyamaze katika kanisa, simruhusi kunena," na kadhalika. Sasa angalia.

58 Bali, ona, yote hayo ni, ni kuyaanika yote ikiyaonyesha kwa mfano, kama Bibilia yote, Mungu akiungana na Mke aliyekombolewa, Bibi-arusi ambaye Mungu alikuwa naye katika akili Yake kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Hiyo ilikuwa ni tabia za Mungu, zikidhihirishwa. Na sasa kumfanya mtu ambaye angeweza kumkomboa mwanamke huyu, ilipaswa iwe ni kitu kikubwa zaidi kuliko yeye, kipate kumkomboa. Na je! uliwahi kuona . . . mimi—mimi . . . hili huenda likawa . . .

59 Sasa kama baadhi ya ndugu zangu wa Amenia walivyo, fu—fundisho ambalo ni la kisheria, wasingekubaliana, hebu tu mimi ni ninii tu . . . Samahani kwa muda kidogo, naweza kuelezea hili. Kama Yeye ndiye huyo Mkombozi . . . Sisemi hili kuumiza sasa, au kuwa tofauti; Sihubiri fundisho, bali hebu niwaulize jambo fulani.

60 Kama Yeye ni Mkombozi, Yeye alikuja, *kukomboa* ni "kuinua kile ambacho kimeanguka," kukomboa kukirudisha mahali ambapo kilikuwa hapo mwanzo, kwa hiyo hakuna watakaoinuliwa ila wale waliokuwa katika mawazo Yake kule mwanzo. Yeye alikuja kukomboa, siyo hiki chakula cha mzinga tunaoona hapa na pale wanaokiri kuwa Wakristo; bali wale aliokuja kukomboa, ambao walikuwa kwenye mawazo ya Mungu hapo mwanzo. Hawa wengine ni kitu kilichochanganywa kuonyesha kile Kimo. Unaona? Ni ninii tu . . . ni—ni bustani, bustani ya maua. Hiyo inatimiza sehemu yake. Bali kile Kimo ndicho unachotaka kuona, Kimo cha Kristo, ambacho kilikuwa

ni Mungu aliyejitokeza duniani katika umbo la Mwanadamu. Amina! Hicho ndicho Kimo unachotaka kuona. Hicho ndicho. Hawa wengine ni sehemu tu za kujitengenezea, mnaona.

61 Sasa, hii iliakisi tabia Yake ya upendo, ya uungwana, Mungu akiakisiwa katika Mwanadamu aitwaye Kristo. Alikuwa ni Yeye pekee ambaye angaliweza kutenda hili. Hapakuwa na mtu mwingine Mbinguni angeweza kutenda hili, ona, alikuwa ni Mungu. Yeye alikuwa ni ile asili isiyo na dhambi. Yeye alikuwa ndiye lile Neno, asili isiyo na dhambi ya Mungu. Yeye alikuwa ni lile Neno lililodhihirishwa. Ambapo, hilo Neno lilikuwa ndio ule mwanzo.

62 Na kama uko kwenye Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo, ulikuwa dhihirisho la Mungu kutoka kwenye wazo Lake. Yeye alikuona na aliona shauku yako, kabla hata hakujakuwa na atomi, au chochote kile, au chochote kingine, na wewe ni wazo Lake lililofanyika neno, na kudhihirishwa ukawa kile ulicho sasa. Amina. Huyo ni Mungu, ndani yako, akimuakisi Kristo leo. Mnaelewa ninalomaanisha?

63 Sasa, natumaini hilo halitaingiliana na jambo lolote, mnaona, nami nisingependa kusema lolote kinyume cha yale mliyofundishwa.

64 Bali tu ili kwamba mpate kuelewa jambo ninalojaribu kufikia hapa, kuakisi, yakupasa ujitambulishe. Na endapo umejitambulisha, nawe ulikuwa katika mawazo ya Mungu kule mwanzo, ona, na ulikuwa uakisi Wake hapa duniani, utashuhudia ya Kimbinguni, na kama Yeye alivyoshuhudia ya Kimbinguni, pia. Na wakati Yeye alipofufuka kutoka kaburini, na akapewa mwili; sisi, tutakapofufuka, tutakuwa na mwili kama mwili Wake Mwenyewe wa utukufu.

65 Ufufuo ni wa hakika. Ni hakikisho, nasi tuna arubuni yake sasa, wakati Roho Mtakatifu anapoingia na kututambulisha kama mtu wa Mungu aliyekombolewa. Amina! Wakati unapompokea Roho Mtakatifu, unatiwa muhuri mpaka safari itakapokwisha. Hiyo ni ishara yako unayoshikilia, inayoonyesha kwamba ninii yako—nauli yako imekwishalipwa. Wewe ni mtu aliyekombolewa. Shetani hana shughuli na wewe, hata kidogo. Chukua tu ishara yako na umwonyeshe, "Uponyaji wangu umelipiwa. Safari yangu ya kwenda utukufuni imelipiwa."

66 Ishara ni kitu unachotumia kupanda basi la safari au ndege. Tiketi yako ndiyo ishara yako. Unaona?

67 Chukua ishara yako; wewe umekombolewa; ile Baraka, Roho Mtakatifu. Na kama Shetani akijaribu kusukumia kitu Fulani juu yako, muonyeshe tu *Hii*. Hicho ndicho kitambulisho chako. Amina. Umetambulishwa katika kufufuka kwa Kristo. Unatambulishwa katika kifo Chake wakati ukifa; unatambulishwa katika kufufuka Kwake. Na, kwa hilo, inakutambulisha wewe, kwamba ulikuwa pamoja na Yeye kabla

ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, maana umekombolewa, hiyo ni kusema, "umerudishwa." "Wote alionipa Baba watakuja, na hakuna mtu awezaye kuja Kwangu isipokuwa Yeye Baba amenipa huyo, unaona, tangu mwanzo."

68 Sasa angalia, Yeye alikuwa mwenye dhambi . . . asiye na dhambi, kupachukua mahali pa mwenye dhambi, kile kiuasumu. Yeye hakuwa na dhambi ili kwamba aweze kuwakomboa wenye dhambi. Mungu alidhihirishwa ndani Yake na akajitambulisha mwenyewe sawasawa ndani Yake. Sasa angalia.

69 Unasema, "Ndugu Branham, je! ulisema, 'Mungu alijitambulisha Mwenyewe'?" Yeye alifanya hivyo.

70 Sasa, "Hapo mwanzo," kasema Yohana Matakatifu 1, "kulikuwako Neno, naye Neno alikuwa kwa Mungu." Sasa Neno yapasa liwe wazo kabla halijawa Neno, maana Neno ni wazo lililotamkwa. "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwa kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu," mnaona, "alikuwa Mungu. Naye Neno, Neno, alifanyika mwili akakaa kwetu."

71 Kutambulishwa vipi? Sasa Waebrania 4, ona, "Neno la Mungu lina ukali, tena nguvu kuliko upanga uwao wowote ukatao-kuwili ukigawanya," lakata kwenda na kurudi, "lakata hata kugawanya, tena huyatambua mawazo na makusudi ya moyo." Na wakati Yeye alipotenda hilo, hivyo ndivyo manabii walivyotambulika, kwa sababu wao . . . Mungu angenena na kuwaambia tu yaliyokuwa yamekwenda kombo na yaliyokuwa yakiendelea. Unaona? Hicho ndicho kitambulisho cha Neno la saa hii, likidhihirishwa.

72 Yeye alikuwa utimilifu wa Neno la Mungu, kwa maana alikuwa utimilifu wa Uungu kwa jinsi ya mwili. Alikuwa Mungu katika umbo la mwanadamu, na ilimhitaji Mungu kudhihirisha tabia kama hii. Na kisha hayo maisha ya kupendeza yalipaswa yaondolewe Kwake, ili kwamba Yeye aweze kuwaokoa hawa ambao kujua kwa Mungu tangu zamani kuliwaona kule mwanzo, ambao walikuwa ni mawazo Yake kukuhusu wewe na mimi. Yesu alikuja kufanya hilo; maisha Yake makamilifu ilibidi yatolewe dhabihu, kumkomboa huyo mtu. Basi, kama yatafanya hivyo, na wewe ulikuwa pamoja na Mungu katika mawazo Yake hapo mwanzo, unawezaje kukana Neno lake kuwa ni kweli, wakati wewe ni sehemu ya Neno Lake. Amina. Bila shaka. Kuthibitishwa, sawasawa, pasingeweza kuwa na kosa kuhusu jambo hilo. Yeye alisema, "Si mimi ninayetenda zile kazi, ni baba Yangu anayekaa ndani yangu."

73 Sasa tunaona kwamba katika mchafuko mkuu wa siku hii, watu, katika kumwelewa Mungu, "Mungu katika nafsi tatu?" Mungu, ni sifa tatu za Mungu, kama huduma tatu: Mungu juu yetu, katika Roho Mtakatifu juu kule, katika nguzo ya moto; Mungu aliyefanyika mwili na kukaa kwetu, Mwanadamu

ambaye tungeweza kumgusa na kumshika; sasa ni Mungu ndani ya Kanisa. Mungu juu yenu; Mungu pamoja nanyi; Mungu ndani Yenu. Mnaona, Mungu yuleyule, katika madhihirisho matatu mbalimbali, bali ni Mungu yuleyule wakati wote.

74 Angalia, pasiwe na kosa lolote. Asili Yake ya kutokuwa na dhambi ilidhihirisha Neno la Mungu. Na njia pekee ambayo wewe utaweza kudhihirisha Neno la Mungu, kwamba unaliamini na kuliona likitenda kazi nyuma yako, itakubidi uwe na hiyo asili isiyo na dhambi inayotoka kwa Mungu. Kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, ulitambulishwa pamoja Naye. Kabla Neno halijaweza kujidhihirisha Lenyewe kupitia kwako, inachukua asili isiyo na dhambi kutenda hilo.

75 Sana sana, mpaka, Yeye alikuwa Neno kwa utimilifu. Neno la Mungu lilitiririka kupitia ndani Yake kwa urahisi sana hata Yeye angeweza kunena Neno, lingeumba. Unaona, hilo lilionyesha Huyo alikuwa ni nani. Ni nani awezaye kuumba, isipokuwa Mungu? Unaona, Mungu ndiye muumba pekee aliyeko. Naye alikuwa katika upatanifu mkamilifu sana, Yeye na Neno walikuwa pamoja kikamilifu sana, mpaka Yeye aliumba, hata Yeye alikuwa, Yeye na Neno walikuwa mmoja.

76 Hakuna asili nyingine ingeweza kutenda hili. Hakuna asili nyingine ambayo ingeweza. Hakuna mtu, hakuna chochote Mbinguni, hakuna chochote kingine, kingeweza kutenda hilo ila Yeye, kwa maana Yeye alikuwa mwanzo wa hiyo Tabia, Mwokozi! Malaika hakuzaliwa Mwokozi; Yeye aliumbwa Kiumbe cha kumwabudu Mungu, sio Mwokozi. Bali ndani ya Mungu kulikuwamo Mwokozi. Mwanaume wa kawaida aliyezaliwa na mwanamke wa kawaida asingeweza kuwa Mwokozi, sababu asili yake ni ya kimwili. Bali ilichukua Mungu, Mwenyewe! Amina. Na—natumaini mnaliona. Tazama, hilo lilikuwa ni dhihirisho, kudhihirisha Tabia kama hiyo. Kwa wengine, ilikuwa ni mtu aliyeanguka; hakuna chochote kingeweza kuokoa. Malaika hawakuumbwa kwa ajili ya jambo hilo. Mwanadamu alikuwa ni mtu aliyeanguka. Tazama, mtu huyu angeweza . . .

77 Tazama, kuonyesha ni wale ambao Yeye aliwawazia, mawazo Yake ndio Mkristo wa leo, yale mawazo kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu. Sasa kumbuka, "Mwanadamu, wakati alipozaliwa katika dhambi, akaumbwa katika uovu, akaja duniani akisema uongo." Je! hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mhariri.] Hakuna chochote ndani yake hata kidogo. Kwa hiyo, mnaona, kama alikuwa katika mawazo ya Mungu wakati alipokuja duniani, yeye amekuja (katika mawazo ya Mungu hapo mwanzo) kudhihirisha tabia Yake. Je mnanielewa? ["Amina."] Ndipo Yesu alikuja kuondoa mawingu, ili hiyo tabia iweze kujidhihirisha yenyewe. Amina. Jambo ndilo hilo. Yeye ni Neno la Mungu lililodhihirishwa. Sasa, hakuna kitu kingine chochote ambacho kingeweza kuwa kinajidhihirisha;

watu wengine wote walikuwa wameanguka. Ndipo, mnaona, je! Yesu alikuja, kuwarudisha watu hao? Hapana, hapana, walizaliwa katika dhambi wakaumbika katika uovu.

78 Yeye alikuja kama Mkombozi na *kukomboa* chochote, ni "kukirudisha." Amina. Kukirudisha! Lilikuwa ni wazo la Mungu, wewe! Fikiria! Maskini wewe, maskini mimi; hakuna yeyote ulimwenguni angeweza kuchukua mahali pangu, hakuna anayeweza kupachukua pako. Wewe ukiwa Mkristo na umejazwa Roho, Mungu, na kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, alikuona na alijua kila umbo ulilonalo, unaona, na Yesu alikuja kukurudisha. Ndio maana Yesu alikuwa hapa, yule Mkombozi, ule mwili wa kibinadamu, ili kukurudisha. Ilibidi Huyo aje kama mwanadamu, kama Mkombozi, kudhihirisha tabia Zake kama Mwokozi, akaja kukukomboa na kukurudisha mahali ulikotoka. Wewe ulikuwa . . .

79 Wakati unapopokea Uzima wa Milele, kuna aina moja pekee ya Uzima wa Milele. Hilo ni neno la Kiyunani, *Zoe*. Ni kweli, ndugu? [Huyo Ndugu anasema "Ndio."—Mha.] *Zoe*, "Uhai wa Mungu Mwenyewe." Kwa hiyo wewe, ukiwa ni mwana, unafanyika sehemu ya huo Uhai. Kwa hiyo ule Uzima ulio ndani yako kamwe haukuanza wala Huo kamwe hauwezi kwisha. Wazia hilo. Huo hauwezi kwisha, kwa sababu chochote ambacho ni cha Milele kamwe hakikuanza. Ule Uzima ulio ndani yako kamwe haukuanza, hiyo ni kusema, kama unao Uzima wa Milele. Na huyo ni Mungu, kwa maana ulikuwa katika wazo Lake tangu Milele, na sasa linadhihirishwa hapa katika mwanadamu, kwa ajili ya utukufu Wake. Yesu alikuja kuwakomboa hao, akiwa ni Mwana, utimilifu wa Mungu ilipasa uje na kufanyika hilo. Ile tabia ya Mungu isiyo na dhambi ilitenda hilo, ili kwamba apate kukomboa haya mawazo mengine ambayo yalikuwa yaje Kwake, kumleta Mke. Mnaona ninalomaanisha? Loo, ni hadithi ya utukufu! Sisi hatuninii . . . hatupaswi kuingilia hilo, kwa vyovyote. Hebu tuendelee. Vema.

80 Angalia, "kuumbwa." Mungu, Mungu alitiririka kupitia kwake jinsi tu u—upepo ungevuma kupita kwenye—kwenye jengo, au kama maji yanavyotiririka kama kijito, hata Yeye alikuwa . . . Yeye na Neno wakiwa Mmoja. Hakuna mtu mwingine angeweza kutenda hilo, kwa maana Yeye alikuwa Ndiye pekee ambaye alizaliwa bila kujuana kimwili. Wengine wote walizaliwa kwa tamaa ya kujuana kimwili, kwa jinsi ya mwili. Yeye alizaliwa pasipo tamaa ya kujuana kimwili. Yeye alizaliwa na bikira.

81 Mungu alijitambulisha Mwenyewe kama tulivyo sisi. Yeye alichukua—alichukua asili Yake, kile Yeye alichokuwa, asili Yake kama Mungu, na akatandaza hema Lake hapa chini na akafanyika mwanadamu. Yeye alijitengenezea hema, mwili wa kuishi ndani yake, na huo mwili unajulikana kama Yesu. Mungu aliishi ndani ya Kristo. Unaona, Yeye alifanyika mwanadamu,

ili atuokoe. Na Yeye alichukua ninii yetu juu yake, umbo letu, ili Yeye aweze kuumba ndani yetu tabia Yake.

82 Na tabia Yake ilikuwa, kwamba, Yeye alitenda kila kitu ambacho kilimpendeza Mungu, na Yeye alidumu na Neno. Yeye alitutaka kwa ajili hiyo kwamba, tungedumu na Neno la Mungu, tutafute mahali petu, na kisha tujue tulikokuwa. Tudumu na Neno Lake! Na, wazia hilo, tumeitwa kufinyanga tabia yetu wenyewe iwe Yake. Sasa tutaona jambo ambalo tumetenda. Kufinyanga tabia zetu kuwa kama Yake Mwenyewe, kwa Roho Wake Mwenyewe. Kisha sisi, kwa njia Yake, ni wana wa Mungu, jinsi tu nilivyoelezea, kwa kuwa na akili Yake ndani yetu, kufinyanga tabia yetu iwe kama Yake, nia Yake. “Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu ambayo ilkuwamo ndani ya Kristo.” Kama nia hiyo ikiwa ndani yako, basi, unaona . . .

83 Yeye alitenda lile tu ambalo lilimpendeza Mungu. Yeye alijijua Alikuwa ni Nani. Alikuja, Mwana wa Mungu. Yeye alijua alikuwa apachukue mahali hapo. Tabia Yake ilipasa iwe hivyo. Na ndipo wakati Yeye, akiisha kuchukua mahali hapa, Yeye alijua mambo yaliyompasa Masihi, naye daima alimtafuta Mungu kwa kufanya mambo hayo, na hakutenda lolote mpaka Baba alipomwonyesha.

84 Sasa kama ukipata mahali pako, dada, hebu nisikuudhi, au ndugu, bali utapata mahali pako katika Neno, kama Mkristo. Sio kile kanuni ilisema; hizo ziko hapa chini katika chambo hii ya kiwango cha chini zaidi ambayo inakwenda kuangamizwa. Ona, wewe tafuta mahali pako kama Mkristo, kwa sababu tabia yako imeumbika kama ya Kristo. Wewe ni *Zoe* namna ile ile kama Yeye alivyokuwa *Zoe*. Basi kama Biblia imesema “Mwanamke asikate nywele zake,” unawezaje kutenda hilo? Inasema “mwanaume ni mtawala wa nyumba,” ninyi wanawake mnawezaje kuwa? Mna shida gani enyi wanaume ambao ni wana wa Mungu? Mnaona? Mnaona, hampati mahali penu. Mnaona? Hebu angalieni sasa. Katika . . . Mnakaribishwa kuja na kuchukua tabia Yake. Unapokuwa na tabia Yake ndani yako, inakuumbia nia ile ile iliyokuwa ndani Yake, na nia Yake ilikuwa sikuzote ni kutenda yale Baba aliyokuwa ameamuru Yeye ayatende.

85 Alisema, “Yachunguzeni Maandiko. Hayo yananishuhudia Mimi.” Kwa maneno mengine, “Kama sitendi sawasawa na vile Maandiko yamesema nitende, basi nionyesheni Mimi ni wapi sikutenda hivyo.”

86 Sasa vipi kama Mungu alisimama jukwaani leo, na kusema, “Mkristo anatakiwa afanye nini?” Basi sisi sote tungelikuwa wapi? Unaona, ile tabia haijidhihirishi yenyewe.

87 Nia Yake ilikuwa ni kudumu na Neno la Baba Yake. Nia za—zao zilikuwa ni kuninii . . . Nia ile ile iliyokuwa ndani yao ilikuwa iwe ndani yetu. Na kama nia Yake iko ndani yetu, tutatenda

kama Yeye alivyotenda. Kama tabia Yake imo ndani yetu, tutakuwa kama Yeye alivyokuwa. Je! hilo ni sawa? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Manabii wote walikuwa na hiyo, tunajua. Tulimchukua, mchukue Nuhu, jinsi alivyotenda katika siku yake, Musa, jinsi alivyotenda katika siku yake, Danieli katika siku yake, wana wa Kiebrania, na kadhalika.

88 Neno huumba tabia ya Mungu kwetu, na chochote kinachojaribu kuchanganyishwa na hiyo tabia, huvunja lile umbo. Huwezi kuchanganya kanuni ya imani na Neno. Hawezi kuchanganya ulimwengu na Neno. Yesu alisema, “Huwezi kumtumikia Mungu na mali.” *Mali* linamaanisha “ulimwengu.” Huwezi; ni moja ama nyingine. “Mkiipenda dunia, ama mambo yaliyo katika dunia, kumpenda Mungu hata hakumo ndani yenu.” Je! hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Basi, mnaona, hamwezi kulichanganya.

89 Huwezi kuchanganya mafuta na maji. Hayatachanganyikana. Unaweza kuyakoroga juu chini, utende lolote unalotaka, hayatachanganyikana.

90 Na tabia yako haitachanganyikana na ulimwengu, kama unaumbwa katika umbo la Mungu, kwa kuruhusu ile nia iliyokuwa ndani ya Kristo iwe ndani yako. Huo ndio mnara wa kuongozea, mwelekeo.

91 Sasa hebu na tutazame katika kioo cha Mungu, Neno Lake, na tutambulishe tabia yetu ya sasa kwa mtu fulani wa Biblia. Nasi tutafunga tu katika dakika chache sasa. Jitambulishe mwenyewe. Sasa *Hiki* ndicho kioo unachotaka kufanya kama huyo mvulana mdogo alivyofanya, ujitazame. Hebu na tutazame ndani ya *Hiki* na tuone kama tunaweza kujiona tukiakisiwa na mtu fulani wa Biblia. Tuone walivyotenda katika hali fulani, na tuone tunavyotenda sasa. Basi nisikilizeni kwa makini sasa, uone namna ya tabia yako ya sasa ilivyo kama Mkristo.

92 Sasa unaweza kuhukumu. Hilo halitafanya mtu yeyote akuhukumu; wewe jihukumu mwenyewe, unaona. Hakuna anayekuhukumu. Mimi sipitishi hukumu. Bali hebu tu tutafakari, tuone jinsi inavyoakisi kutoka kwenye watu fulani wa Bibla, tunapowataja, na uone tabia yako ilivyo wakati huu wa sasa. Sasa angalia, Ne—Ne—Neno huumba tabia, tunajua hivyo, sasa tunatazama katika kioo Chake na kujitambulisha wenyewe na mtu fu—fulani katika Biblia.

93 Kama uliishi katika siku za Nuhu, na ulikuwa na tabia yako ya sasa. . .Kama mnanielewa, semeni, “Amina.” [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Kama ulikuwa unaishi katika siku za Nuhu, na uko katika tabia yako ya sasa, ni upande gani ambao wewe ungekuwa? Uwe mwangalifu, unaona. Katika tabia yako ya sasa; sasa wazia kile ulicho. Wakati makundi. . .Ni kundi gani ungetambulishwa nalo, kama tabia yako ya sasa ingekuwa inaishi katika siku za Nuhu? Je! Ungekuwa na yule nabii na

Neno la Mungu lililothibitishwa, ukisimama katika uchache, lile kundi dogo, au ungekuwa na jamaa wenye maoni ya watu wengi wa siku hiyo? Tabia ipi?

94 Je! ungekuwa mshirika wa makanisa, na kadhalika, waliokuwa wanamfanyia dhihaka yule nabii juu kule? Ungekuwa unatembea na kundi lililopanda juu na kusema, "Vema, sina jambo lolote dhidi ya huyo mzee; anaweza kuwa sahihi," au ungekuwa mle ndani ukipaka rangi lami pamoja naye? Sasa wazia tabia yako sasa. Ungefanya nini wakati kila kitu kilikuwa dhidi ya hilo?

95 Kumbuka, ulimwengu ulikuwa unamlaumu yule nabii na ujumbe wake, na—na kila kitu, ulimwengu, alilaumiwa. Makanisa yote yalikuwa yanamlaumu. Sayansi yote ilisema, "Mtu huyo ni kichaa." Kama walivyosema kumhusu Yesu, kula nyama na kuinywa Damu Yake, walisema, "Mtu huyu ni mla watu. Yeye ni kifyonza damu." Unaona? Kwa hiyo mnaona walipo hao wenye busara, tunaowaita watu wenye busara wa ulimwengu, wale wanasayansi?

96 Je! ulijua, wakati unapopata elimu zaidi na ustaarabu zaidi, ulijua kwamba hayo yanakuweka upande gani? Hayo yanakuweka upande wa ibilisi. Biblia ilisema ya kwamba, "Wana wa giza wana hekima kuliko wana wa nuru."

97 Watazame wana wa Kaini, kila mmoja wao alifanyika mwanasayansi, wenye kushughulika na majengo, na kufanya maendeleo makuu. Bali wana wote wa Sethi walikuwa wanyenyekevu, wakulima wadogo, wachungaji. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Watu hodari, wa zamani, kama ilivyokuwa katika siku za Nuhu, jinsi walivyojenga na kutengeneza, na kujenga piramidi na kila kitu, wanasayansi. Angalia kwa makini sana sasa, unaona. Hawa watu walikosoa ujumbe wa huyu mtu, japokuwa alikuwa na ushahidi wa Mungu.

98 Au vipi kama ungeliishi katika siku za Eliya; Eliya, wakati yeye akiwa mchungaji wa siku hiyo? Na Yezebeli, miaka elfu mbili mia tano iliyopita, Holywood ilikuwa ikianza, na vipodozi vyake vyote na mitindo, alikuwa amewafanya binti wote wa Israeli kufanya jambo lilelile. Na mzee mmoja akisimama pale na kuigongagonga kwa nguvu! Na makuhani wote wakisema, "Loo, vema, maskini jamaa huyo mzee, mwacheni, atafikia mwisho wake baada ya kitambo kidogo. Hana lolote. Naye, mfalme wetu mzuri ambaye amevaa kama tulivyovaa, na tunazo nguo maridadi sana, na taifa linalolishwa vizuri sana, na kila kitu, inaleta tofauti gani kama unatenda *hili*, au *lile*, au *linginelo*? Inaleta tofauti gani?" Wachungaji walikuwa wakisema jambo hilo.

99 Bali hapo alisimama mtu mmoja, peke yake, akiwa na BWANA ASEMA HIVI.

100 Sasa katika tabia yako ya sasa, ungewekwa upande gani wakati huo? Sasa angalia kwenye kile Kioo, wakati utakapokwenda nyumbani utaona uko wapi. Unaona? Unaona? Ni, ni mazingira gani hali yako ya sasa ingekuweka katika siku ile? Je! ungekwenda na wazo la kisasa, la madhehebu, ile ishara, yule jamaa, "Loo, vema, sote tumefunga ndoa"? Loo, hakika, wote walimwabudu Yehova kila mwandamo wa mwezi, na walipiga yowe na kunywa maji kutoka kwenye ile chemchemi na kumtukuza Mungu wa Mbinguni aliyewaleta hapo, na wote namna hiyo, bali wako umbali wa maili milioni moja nje ya mstari. Ni mahali gani uzoefu wako wa sasa wa Ukristo ungekuweka wakati wa Eliya? Ungetambulishwa upande gani? Ungechukua upande gani wakati huo?

101 Au, wakati Musa alipowaleta Israeli, akishuka kwenda kule kama nabii aliyetambulika, pamoja na Neno ambalo Mungu alikuwa amemwahidi nabii Ibrahimu, kuwa lingetimia, basi Musa akashuka na kutenda ishara zote ambazo Mungu alimwambia atende. Sikilizeni kwa makini sasa, tunafunga katika muda mfupi. Aliwatoa hao wana na wakaenda nyikani, ule ujumbe, kama ninyi wapentekoste mlivyoondoka miaka hamsini iliyopita kutoka katika madhehebu, nao walivuka ule—ule mstari kule, na akainuka mtu, kasema, "Sasa hebu kidogo, hebu na tuunde madhehebu kutoka katika huu," jamaa aliyeitwa Dathani. "Musa, unafikiri ni wewe pekee ufukoni. Unafikiri ni wewe pekee mtakatifu miongoni mwetu. Tunao watakatifu wengine, wa kusema jambo fulani kuhusu huu. Tutajifanyia tu kundi dogo, nasi tutaamini kwa *hivi*, na tutamini *vile*, na tutaamini *hivi*."

102 Sasa ni kundi lipi tabia yako ya sasa ingekutambulisha nalo? Je! wewe, katika siku za—za Eliya ungekwenda nje kule mahali ambapo Yezebeli, tuseme, alikata nywele zake na kupaka uso wake vipodozi, na alikuwa mwanamke wa kisasa? Basi wazia tu ni wapi unatambulishwa sasa. Unasema, "mimi ni Mpente . . . " sisemi kile ulicho. Ninaulizia tabia yako. Tunashuka chini ya mambo haya madogomadogo unayoyatazama. Tunaingia ndani yako.

103 Je! ulimsikia Roho mtakatifu usiku uliopita, jinsi hatimaye alivyokaripia kule? Hiyo ndiyo sababu ninasema ninavyosema leo. Unaona? Fungueni ninii wenu . . . ufahamu wa kiroho, enyi watu, tume—tumechelewa kuliko mnavyowazia. Mnaona? Mnaona? Mnaona? Mnaweza. Ni—ni njia ambayo mtu angeweza kufikiri kwamba uko sawa. Bali niliwaza, pengine, kama Bwana angeniruhusu kunena hili, kwamba wangenisamehe kwa hili, shi—shirika hili, au, ndugu; ambapo, najua wanafanya hivyo, wako pamoja nami kwa hili.

104 Angalia. Bali, hili, kama—kama unaweza tu kujiona mwenyewe leo, katika nuru; kama roho yako, iliyokuwa ndani yako, iliishi katika mtu fulani nyuma kule. Sasa angalia

mahali ulipo leo, nawe utaona mahali ungalikuwa huko nyuma. Ungalikuwa wapi katika wakati huo? Je! ungeliungana na madhehebu ambayo Dathani alitaka kuyaunda? Au, je! tabia yako ya sasa ingekutenganisha na hayo, na kudumu na Neno, ona, wakati ilionekana kwamba wote walikuwa dhidi ya hilo?

105 Musa alikuwa amethibitishwa kikamilifu, kwamba alikuwa na ujumbe wa Bwana. Mungu alikuwa ameuthibitisha kwa kila namna, ilivyo sawa kabisa jinsi Yeye alivyosema ilikuwa utimie; aliwaambia Israeli, kule nyuma katika Kumbukumbu la Torati, nyuma kabisa huko, "Chochote ambacho ishara hizi zingekuwa, ni lazima mukifuate na kukisikiliza, na kusikia kile Neno liliahidi." Yeye alidhihirishwa.

106 Na hata hivyo Dathani, kiongozi stadi kule Misri, aliinuka na kusema huko, "Utajaribu kujifanya mwenyewe ni wewe pekee uliye na chochote."

107 Hilo halikuwa wazo la Musa. Yeye alikuwa anatenda tu yale Mungu alikuwa amemwamuru atende. Wote haikuwabidi kuwa Musa. Hao watu walipaswa kufuata tu yale alisema. Haikumpasa kila mtu kuumba, na kufanya miujiza na kadhalika. Hiyo ndiyo shida ya watu leo.

108 Bibi Fulani aliniuliza, nikishuka kuja barabarani, hivi majuzi, kutoka juu hapa. Akasema . . . Ni Florence Shakarian, dada wa ndugu Demos, na Dada Williams na hao wengine wakiwa wameketi ndani ya gari. "Akasema, Ndugu Branham, ninafunga na kufunga na kufunga, na bado siwezi kutoa pepo."

109 Nikasema, "Hukuzaliwa kutenda hivyo. Wajibu wako, ni kufunga. Roho Mtakatifu anatenda kazi na mtu mwingine nje huko kwa jambo hilo. Wewe hujui ni wapi."

110 Kama tungekuwa na wakati, tungefundisha mambo hayo katika mikutano mirefu. Jinsi kwamba mtu mmoja ana mzigo, namna *hii*, kwa ajili ya jambo Fulani *hapa*. Wewe hujui, hujui, na si kazi yako kujua. Ni Yeye anayetenda hilo. Wewe unajisalimisha tu kwa wito wako, na sikuzote unayafuata Maandiko, uone kama ni kweli au si kweli.

111 Sasa tunaona, wote . . . huyu alikuwa ni Musa ambaye alikosolewa, na yeye ali—yeye alikosolewa na kundi hili, lakini Mungu akamwambia Musa, "Jitenge naye, kwa sababu nitammeza katika ardhi," Naye alimmeza. Sasa, unaona, ni lazima ujue saa unayoishi, na kisha uhukumu tabia yako na jinsi walivyokuwa.

112 Au, katika siku za Kristo. Nataka kuwauliza sasa. Wakati walipokuwa na seminari bora sana, wahudumu bora sana, wasomi waliobobea, sherehe za dini zilizo takatifu sana, na kila kitu ambacho sisi, walichowahi kuwa nacho; na wakati Yesu alipojitokeza jukwaani, Yeye kwa kweli alikuwa "haini" kwao. Bali, unaona, Mungu alitambulisha tabia Yake Mwenyewe ndani Yake, kwa kudhihirisha kwamba Yeye alikuwa Mungu.

Na Yeye akasema, "Kama hamjui Mimi ni Nani, yachunguzeni Maandiko."

Kasema, "Tunamjua Musa. Sisi hatu . . . "

113 Kasema, "Kama mngelimjua Musa, mngenijua Mimi. Yeye aliandika habari Zangu."

114 Sasa, kama uliishi katika siku hiyo, na ulikuwa mshirika wa kanisa mojawapo zuri la Baraza la Wazee, mchungaji mzuri, ungechukua upande gani? Upi, ni upande upi tabia yako sasa ingekuweka? Waza. Ni juu yako. Upande upi, ambao tabia yako—yako uliyo nayo sasa, ungejitambulisha wapi katika siku za Yesu, wakati mchungaji wako aliposema, "Loo, hayo mambo ni upuzi?"

115 Na hata hivyo huyu hapa Yesu anarudi, akisema, "Maandiko yalisema ningetenda *hili*," na Yeye akalitenda. "Maandiko yalisema ningetenda *hili*, na 'kuzaliwa kibikira.' Maandiko yalisema ningetenda *hili*," na Yeye akalitenda. Yeye akasema, "Yachunguzeni Maandiko na muone ni wapi nilishindwa."

116 Bali wao wakasema, "Msimjali jamaa huyo; yeye amerukwa na akili Zake." Mnaona?

117 Ipi, ni tabia ipi uliyo nayo sasa? Ungewekwa mahali gani nyuma kule katika siku ambazo Yesu alikuwa duniani, wakati madhehebu makubwa na wanathiolojia wote walikuwa dhidi yake, na waalimu wote na wanathiolojia wa siku hiyo walikuwa dhidi Yake, waalimu wote wa Biblia walikuwa dhidi Yake? Dhidi ya nini? Dhidi ya Neno la Mungu lililo wazi kwa ajili ya wakati huo likidhihirishwa, likitambulishwa, Mungu Mwenyewe akitambulishwa.

118 "Ataitwa Jina lake Mshauri, Mfalme wa Amani, Mungu Mwenye Nguvu, Baba wa Milele. Bikira atachukua mimba na kuzaa mwana huyu. Uweza wa kifalme utakuwa mabegani Mwake, unaona, na ufalme wake hautakuwa na mwisho." Mtu huyu ni nani? Mtoto mchanga, Mungu, na ndipo Mungu anafanyika mwanadamu. Ungeweza kuwazia Yehova akilia kama mtoto mchanga? Ungeweza kuwazia Yehova akizaliwa katika hori? Ungeweza kuwazia Yehova akicheza kama mvulana? Ungeweza kuwazia kanisa fulani, ambalo lilidai kumwabudu Yeye, likimsulubisha?

119 Sasa ni upande gani wewe ungetambulishwa nao? Kile Neno sahihi na la kweli, lililodhihirishwa lililokuwa likinena, Lenyewe, au ungeshikilia kanuni yako? Tabia yako ya sasa, je! ungekuwa wapi? Sasa ungekuwa mahali papo hapo. Vyovyote vile ulivyo sasa hivi, hivyo ndivyo ungelikuwa nyuma kule, huko huko kabisa, waziwazi. Lo, jamani!

120 Wakati, ishara Yake ya Masihi, chunguza sasa, ishara Yake ya Masihi ilitambulisha tabia Yake, kwa maana alikuwa ni Mungu

ndani ya mwanadamu, lile Neno. Unaona ninachomaanisha? Lilipambanua mawazo, na kuwaambia mambo yote haya.

121 [Sehemu tupu kwenye kanda—Mha]...Neno lilimkuta humo. Bali wakati Neno lilipomulika kwa mara ya kwanza, alilipata. Alikuwa ni mmoja wa hayo mawazo ya Mungu, ambayo yalidhihirishwa. Unaona?

122 Bali wale waliosimama pale katika majoho ya kidini, na hadhi ya kila namna, na kila namna ya kupotosha Neno katika vitu mbalimbali, na wakilifanya hilo bila uaminifu, mradi tu walikuwa washirika wa kanisa, ndio waliodai kuwa wana nuru, na ile Nuru ilitia giza ile nuru waliyokuwa nayo.

123 Ni kama tu wewe ukijaribu kushikilia tochi wakati wa jua, kulizimisha jua. Unaona? Kwa nini tochi haitazimisha jua? Kwa nini nuru nyingine yeyote? Hakuna nuru inayoweza kuzimisha jua. Kwa nini? Ni Neno la Mungu lililodhihirishwa. Mungu alisema, "Iwe nuru," na hiyo ni Nuru ya Mungu. Ni Neno la Mungu lililodhihirishwa; huyu hapa anakuja!

124 Hakuna kanuni za imani, madhehebu, hakuna papa, kuhani, au chochote kile, au Daktari wa Uungu, hakuna madhehebu, hakuna taifa, hakuna chochote, kitakachoweza kuzimisha dhihirisho la nuru ya Mungu. Wakati Neno linaponenwa nalo linakuwa Nuru, litafanya kile ambacho lilisema kwamba lingefanya. Hakuna kanuni ya imani inayoweza kusimama karibu Nalo, hakuna chochote kinachoweza kusimama karibu nalo, ila Nuru Yenyewe na hao ambao watatembea ndani yake. Huyo ni Yesu Kristo aliyefufuka katika wafu, akiwa hapa akijidhihirisha Mwenyewe miongoni mwetu, nasi tunatembea ndani Yake. Hakuna chochote kinachoweza kulikomesha. "Mbingu na nchi," Yesu alisema "zitapita, bali Hilo halitapita." Angalia, waalimu wote wa Biblia, na kadhalika . . .

125 Hata hivyo, akiona Neno hilo limethibitishwa, ishara Yake ya umasihi ikimwonyesha yule maskini kahaba kwamba Yeye alikuwa ni Nani, wengine waliokuwa mawazoni mwa Mungu, kama Petro na—na Nathanaeli, na wote wale waliokuwa katika mawazo ya Mungu. Mara tu hiyo Nuru ilipomulika, waliitambua. Haikuwalazimu kuwakokota hadi mimbarani, kuwaita na—na kuwabembeleza, na kuwaambia ungewafanyia jambo jingine kama wangekuja, na ungewapa maisha bora, na uone kama ungeweza kumshawishi bosi wapate kazi, kuwaweka katika mtaa bora zaidi. Wao hawakujali. Iliwabidi kupigana kushikilia mahali pao. "Bali hakuna kitakachotutenganisha," ilisema Biblia, "na upendo wa Mungu ulio katika Kristo." Mateso, hatari, kifo chenyewe, haviwezi kututenganisha, kwa sababu sisi sote tulikuwa, sikuzote tulikuwa, katika mawazo Yake. Vema, tunaendelea.

126 Je! hali yako ya sasa ingekutambulisha na Mafarisayo wa siku hiyo? Je! hali yako ya sasa ingefanya hivyo? Sasa

kama ungesema, “Hapana, isingenitambulisha mimi na hao Mafarisayo wakati huo,” basi vipi kuhusu sasa? Waebrania 13:8 ilisema ni yeye yule jana, leo, na hata milele. Basi ni hali gani ambayo tabia yako ya sasa inakutambulisha nayo sasa? “Nisingekuwa na uhusiano wowote na hao Mafarisayo. Hapana, bwana.” Sasa, hilo ni jina tu, kwako. Bali vipi kuhusu hali uliyo ndani yake, wakati unapomwona Yeye leo katika kanisa Lake jinsi tu alivyokuwa wakati huo, sasa ungelikuwa wapi? Historia inajirudia yenyewe.

127 Mafarisayo wa siku hiyo walisimama dhidi Yake kwa sababu ya chuki. Na hiyo ndiyo shida leo, ulimwengu wa kimadhehebu unasimama dhidi ya kweli ya Neno, kwa sababu ya chuki bila sababu.

128 Nikihojiwa na padri wa Katoliki sio siku nyingi zilizopita, aliniambia, “Unajaribu kufundisha Biblia.”

Nikasema, “Hiyo ndiyo ninayoamini.”

Akasema, “Mungu yuko ndani ya kanisa Lake.”

Nikasema “Mungu yuko ndani ya Neno Lake.”

129 Akasema, “Ilikuwa, watu wote wa awali walikuwa wakatoliki.” Nikasema . . . “Petro, Yakobo na Yohana wote walikuwa Wakatoliki.”

130 Nikasema, “Kama wao walikuwa . . . ” Naye akasema . . . Nikasema, “Wewe, unawazia nini kuhusu kanisa leo?”

Kasema “Ni bora zaidi kuliko lilivyokuwa wakati huo.”

131 Nikasema, “Fanyeni yale mambo mliyofanya wakati huo.” Unaona, tabia inaonyesha kwamba ni kitu gani hasa.

132 Mafarisayo wa siku hiyo, kwa ajili ya chuki! Kumbukeni, ilikuwa ni chuki. Wao kwa kweli waliliona Hilo! Nikodemo, mmoja wa makuhani wao, alieleza hilo, na akasema, “Rabi, sisi tunajua Wewe ni mwalimu umetoka kwa Mungu. Hakuna mtu angeweza kufanya yale ufanyayo Wewe isipokuwa Mungu yu pamoja naye.” Unaona, bali kwa ajili ya chuki, kwa sababu Yeye hakujiunga na kundi lao!

133 Kama Yeye angekuja, aseme, “Sasa ninyi Mafarisayo mmekosea; Mimi ni—Mimi ni Msadukayo,” au, “nyinyi Masadukayo mmekosea; Mimi ni Mfarisayo.” Mafarisayo wangesema, “Mnaona, niliwaambia sisi tulikuwa sahihi.” Bali Yeye hakuja kwa yeyote wao; bali Yeye alisimama kati yao.

134 Kama ungelikuwa unamfuata Yeye, kuona miujiza Yake wakati huo, na kisha . . . Na useme, “Loo, ningependa kuona miujiza Yake.” Nawe ulimfuata Yeye, kuona miujiza Yake.

135 Ndipo basi wakati Yeye alipofika mahali hapa, alisema aliacha kuonyesha miujiza Yake, kana kwamba, na kuanza kuwafundisha. Na wale wahudumu sabini, waliowekwa wakfu na Kristo, waliinuka na wakamwacha kwa sababu Yeye alisema

jambo fulani ambalo sayansi isingeweza kukubaliana nalo, au umati uliosalia wasingeweza kukubaliana nalo. Hawakuweza kuelewa jinsi huyo Mtu, akiwa ni mwanadamu, hata hivyo alijifanya Mwenyewe ni Mungu aliyeshuka kutoka Mbinguni. Mwana wa adamu akipanda juu mahali Yeye alikotoka. Yeye alikuwa Mungu. Hakika, Yeye alikuwa. Wakasema, "Lo, sisi, hilo ni gumu mno, hatuwezi kukubaliana nalo."

136 Ungetambulishwa wapi wakati huo, sasa na tabia yako iliyoumbika ndani yako? Kitu fulani kimeumba tabia yako. Wewe ni tabia ya aina fulani. Ungejiona mwenyewe mahali fulani hapa. Ungefanya nini? Nini, katika hali yako ya sasa, ni nini, ni wapi ungekuwa wakati huo? Unaona?

137 Waalimu wote dhidi Yake, na kila kitu, na miujiza Yake ilimtambulisha Yeye. Na wakati wale sabini walipoinuka, na wachungaji na wahudumu, na waliinuka na kusema, "Hatuwezi kuelewa Hilo," wewe ungaliondoka kama hilo kusanyiko? Au ungalikuwa kama wale wanafunzi, "Sijali wanayosema"? Unaona, liko hapo.

138 Ndipo Yesu akageuka na kuwapa jaribio, akasema, "Nyinyi nyote mnataka kwenda, pia?"

139 Unaona, walikuwa wamemnasa Yeye katika mtego. "Mbona, huyu Mtu ni kizuu kifyonza damu ya watu," wakasema, "yatupasa kula nyama Yake na damu." Wakaondoka, lile kusanyiko.

140 "Vema," wahudumu wanasema, "vema, tutakaa muda kitambo zaidi, tuone yote yanahusu nini."

141 Naye akasema, "Sasa wakati mtakapomwona Mwana wa Adamu akijitambulisha Mwenyewe kama Mungu sasa, unaona, mtakapomwona Mwana wa Adamu akipaa mbinguni mahali Yeye alipotoka."

"Loo," wakasema, "jambo hili limetuzidi mno," nao wakaondoka.

Ndipo basi akawageukia wanafunzi, akasema, "Ninyi mnataka kwenda pia?"

142 Ndipo Petro akasema, "Bwana, twende kwa nani? Twende wapi? Tunajua kwamba Wewe, na Wewe pekee, una maneno ya Uzima."

143 Na ni jambo lile lile leo, "Yeye," sio madhehebu yako, sio kundi lako. Kristo, na Yeye pekee, ana Neno la Uzima. Ni wapi unapojitambulisha mwenyewe, na hadithi fulani ya uongo ya kitu fulani ambacho mwanadamu ametunga, au mafanikio ya Mungu? Kama nilivyonena Jumapili iliyopita juu ya Kuhesabu *Kinyumenyume*, yale Mungu ameweza kufanikisha, kuleta kanisa lake katika wakati wa mwana anga sasa. Mnaona? Au, wewe ungekuwa wapi, au unaweza kuona utambulisho wako mwenyewe sasa?

144 Angalia, ukiwa na mwalimu maarufu, anayekupenda. Nataka kuzungumza nanyi vijana, kwa muda mfupi sasa tu. Unajitambulisha wapi, kijana mwanamke, wewe uliye shuleni? Loo, unaweza kujishughulisha na mambo madogomadogo, unaweza kuonyesha yote *haya*, na—na wewe ni mwalimu wa sayansi na kila kitu. Bali unajua nini? Hayawezi kukupa uzima.

145 Uzima huja tu kwa njia ya Kristo, "kumjua Yeye," sio kujua Neno Lake, sio kujua Kanisa Lake, sio kujua *Hili* Lake. "Kumjua Yeye," hilo ndilo jambo pekee linaloweza kukupa uzima.

146 Na sasa wakati Hili linapokuja mbele ya tineja, kitu kama mvulana wenu wa kisasa wa Kipentekoste, Elvis Presley, aliyeuza haki yake ya mzaliwa wa kwanza kwa ajili ya kundi la makadilaka na santuri za dhahabu za mamilioni ya dola, na kadhalika. Hilo ndilo ulimwengu unataka. Wanataka Pentekoste inayoweza kuruhusu wa—watu . . .

147 Leo, wanawake wanataka Pentekoste itakayoru—itakayowaruhusu kukata nywele zao na kuvaa kaptura, au kutenda chochote wanachotaka, na—na washikilie tu ushuhuda wao—wao wa kuwa ni Wapentekoste. Wao, wao wanataka hilo namna hiyo hiyo. Unaona? "Hapana, nisingalikwenda kwenye kundi hilo. Hapana, wao wana . . . Huo ni mtindo wa kale." Unaona? Unaona, wanapenda hilo. Ni ile asili tu. Na baadhi ya wanaume hao, wanaoongozwa na wanawake, wamewapatia hilo.

148 Lakini, "Mungu anaweza katika mawe haya." Mtu fulani anapaswa kusambaza ile Nuru, na tuna mtu leo ambaye haogopi kuisambaza, pia. Hebu na iwe chochote inachotaka kuwa.

149 Unatambulishwa wapi, uko na kundi gani? Unaona? Unasimama wapi? Angalia.

150 Huyu jamaa mdogo, alijitambulisha na kanisa lake; gharama ilikuwa ni kubwa mno. Kwa hiyo kama—kwa hiyo kama unakumbuka kitambulisho chake cha mwisho, mahali tulipomtambulisha huyu mtawala kijana ambaye alikuwa na nafasi ya kuja kumfuata Yesu. Yeye aliendelea mbele na kuchukua kanisa lake na kusonga mbele. Yeye alikuwa mvulana mzuri, kasema alishika zile amri na kutenda mambo yote haya. Naye alijua vema kama yeyote ya waliosalia, kwa hiyo angechukua tu hilo wazo. Yeye alikataa kumfuata Yesu, na utambulisho wake wa mwisho, tunamwona katika kuzimu, alikuwa akimlilia Lazaro aje na kumletea maji anywe.

151 Au, utambulisho wako, ungeweza kutambulishwa na lile kundi ambalo Yuda alikuwa ndani yake? Alianza kutembea na Yesu. Alianza vema, kama Wapentekoste walivyofanya miaka iliyopita. Bali kitu kile kile walichotoka ndani yake, yale madhehebu, mama na baba zenu, hili kundi changa limegeuka nyuma moja kwa moja na kujiundia moja kama tu lile walilotoka ndani yake. Unaona? Ni kundi la aina gani uko nalo?

152 Sasa Biblia ilisema huu Wakati wa Kanisa la Laodokia . . . Yuda, mnajua, alibeba nini . . . Aliona uwezekano wa kupata kitu fulani kikuu kwa kile alichokuwa nacho. Yeye alitambulishwa pamoja na Yesu. Kwa hiyo aliwazia, kwa huo, yeye alibeba ule mfuko, naye angeweza kutengeneza pesa za ziada kwa kumuuza Yeye kwa vipande thelethini vya fedha.

153 Hilo ndilo kabisa Wakati wa Kanisa la Laodokia ulivyotenda. Biblia ilisema hivyo. "Wewe ni tajiri, nawe unasema, 'nimejitajirisha, na nina mali nyingi, wala sina haja ya kitu.' Nawe hujui kuwa wewe ni mwenye mashaka, maskini, kipofu, uchi; nawe hujui hilo." Hilo ni Pentekoste, Wakati wa Mwisho wa Kanisa; sio Luther, sio Wesley. Bali, Wapentekoste, huo ndio Wakati wa Kanisa.

154 Umetambulishwa wapi sasa? Wasema, "Mimi Mpentekoste." Unaona mahali linakotambulishwa? Kwa kumweka Yeye nje. Hakika, kwa sababu wao ni matajiri, hawana haja na . . .

155 "Lo, mnasema 'matajiri'?" Mbona, mlikuwa mkisimama nje hapa na kulipa dola tatu kwa wiki kwa ajili ya kibanda kidogo pembeni. Sio kwamba najaribu kutambulisha hilo; bali kama inachukua hilo kuhubiri Maneno yote, chukueni hilo. Hakika. Sasa tunalipa dola milioni hamsini kwa ajili ya seminari, na vikundi, na mambo makubwa mno, na kwa sehemu zingine kutumia mabilioni na mamilioni ya dola katika majengo makubwa mno, kutengeneza njia, na tunahubiri kwamba Yesu yuko karibu kuja. Na wamishenari ninaowajua, walio hudumani, hawana viatu miguuni. Amina. Tulipokuwa tukitoa sadaka, wamishenari zaidi; na ndugu mmoja mzee asiye na kitu miguuni mwake bali jozi ya malapa, ndizo tu alizokuwa nazo, alizichukua na kuziweka juu pale katika sadaka kwa ajili ya mmishenari mwingine. Lo, jamani! Unatambulishwa wapi?

156 Wapentekoste! Sitadumu sana hapo, bali mnajua ninalomaanisha. Loo, jamani! Tumeuza! Tumeuza nini? Tumeuza haki zetu za mzaliwa wa kwanza kwa ajili ya kupendwa na watu. Tulitaka kuwa kama Wamethodisti. Mlitaka kuwa kama Wabaptisti na Wapresbiteri. Hayo ndiyo aina ya majengo mliyo nayo. Mnajenga seminari, na kama mtambo wa kuangulia, na kuangua baadhi ya wahubiri watakaowaruhusu kutenda lolote mnalotaka, na bado mjiite wenyewe "pentekoste." Huo ni uongo. Kweli! Kumbukeni, kumbukeni hicho ndicho hasa kilichomgeuza Yuda kupendwa na watu miongoni mwa wahudumu wengine, alimuuza Huyo kwa vipande thelathini vya fedha.

157 Yeye, kitu gani kilimfanya ageuke? Kwa kweli alishuku madai ya Kristo kuwa Neno. Angeweza kumwona huyo Mtu, akala pamoja na Yeye, akavua samaki pamoja na Yeye nje kule, na kila kitu kingine; na Huyo kuwa ni Neno, asingeweza kuamini hilo. Asingeweza kuamini kuwa Yeye alikuwa Mungu; bali Yeye

alikuwa. Tabia ya Yuda ilimsababisha yeye kutenda hili. Je! tabia yako imetenda jambo lilelile? Kumbuka, Yuda alikuwa wa kidini sana.

158 Nilikwenda Afrika, nao wakasema, "Mbona, Elvis Presley, tunazo nyimbo zake pote hapa, yeye huimba."

159 Pat Boone na wengine, hawapaswi kuruhusiwa kulitaja lile Jina. Ufisadi na uchafu! Ni unafiki. "Yeye anayelitaja Jina la Kristo, na ajitenge mwenyewe na dhambi." Unaona? Bali mpo hapo. Mnaona tumefika wapi? Dhambi ni danganyifu mno, huingia kwa hila mno, mpaka hujui kama iko hapo mpaka imejifiringisha kwako, unaona, kisha inakubana. Unaona utambulisho wa mwisho wa Yuda ulikuwa nini?

160 Na, ndugu yangu, kwa sababu kanisa unalohudhuria ni kubwa kuliko hilo lingine pale pembeni, hata hivyo wanahubiri Kweli, nanyi hamfanyi hivyo, unaona hilo linakufikisha wapi? Hiyo ndiyo ile roho ya Yuda. Na je! unajua utambulisho wake wa mwisho? Ulikuwa kujitundika juu ya mkuyu.

161 Au unajiona mwenyewe umetambulishwa na wanafunzi halisi wa Kristo? Sasa tutafunga, hakika bila shaka sasa. Mkweli Kwake na Neno Lake mbele ya lawama zote! Je! unaweza kujitambulisha na Petro kwenye ile siku ya Pentekoste?

162 Wakati wote waliona hiyo, kasema, "Tazama hili kundi la wenda wazimu. Wote wamelewa."

163 Petro alisimama na kusema, "Enyi watu wa Yerusalemu, nanyi mnaokaa Uyahudi, lijueni jambo hili, mkasikilize maneno yangu. Sivyo mnavyodhani watu hawa hawakulewa; hii ni saa tatu ya mchana. Lakini jambo hili ni lile, Maandiko, yaliyonenwa na nabii Yoeli." Ilikuwa ni nini? Neno la Mungu lilikuwa likidhihirishwa. Akasema, "Tubuni, kila mmoja wenu, na mkabatizwe katika Jina Lake Yesu Kristo kwa ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu. Ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali." Ni wangapi? "Na kwa wote watakaoitwa na Bwana Mungu wetu wamjie." Yeye kamwe hakuwaita wote, mnajua. Bali hao, walioitwa, wanajua la kutenda. Vema. Vema.

164 Au, pamoja na Paulo, au wakati wewe ulipokuwa na Paulo hapo De—De—Dema aliyependa kujipendekeza alipomwacha, kwa ajili ya mambo ya ulimwengu, msaidizi wake; laiti ungeliwaona watu wote wakimchekelea Paulo, usikie Paulo akisema, "Nileteeni koti." Mtu mwenye huduma kama aliyokuwa nayo, na alikuwa na koti moja tu.

165 Mbona, Dema aliwaza, "Alipaswa awe na shule kubwa mno ya Biblia na mambo yote haya ya kimadhehebu kila mahali, na awe katika shirika fulani kuu. Mbona, yeye angeweza kuponya wagonjwa. Yeye alikuwa nabii. Mbona, anapaswa kuwa na aina zote za pesa, mamilioni ya urithi, na hapa mtu huyu ana koti moja pekee."

166 Kasema, "Baridi inaingia hapa. Mwambie alete koti langu wakati atakapokuja."

167 Na Dema, alipoona hili, alikwenda na ulimwengu, na kumwacha maskini ndugu yake ajitegemee. Ungethubutu kusimama na umwone Yesu nje kule, akisikia baridi, umwone Yeye akiwa mhitaji, na uondoke na kumwacha?

168 Mnakumbuka Mtakatifu Martin? Wengi wenu ninyi ndugu mnamkumbuka, maandishi ya Mtakatifu Martin. Yeye alikuwa Tora, Ufaransa, naye hakuwa Mkristo. Mama yake alikuwa Mkristo. Alikuwa binamu wa—wa Ireneo. Na, halafu, hii ilikuwa ni miaka mia kadhaa baada ya kifo cha wale mitume, wakati walikuwa bado wanajaribu kuliweka Neno pamoja; na lile kanisa la Katoliki walikuwa wanaliingiza katika mafundisho ya sharti, nao wasingelivumilia hilo.

169 Ndipo Mtakatifu Martin, akipitia katika lango, mahali . . . adhuhuri yenye baridi, na kulikuwa na maskini ombaomba amelala pale, akiganda kwa baridi. Hakuna mtu yeyote angempa koti. Mtakatifu Martin alivua koti lake mwenyewe, akalikata nusu kwa nusu na kumfunika ombaomba huyo kwa hilo, kisha akaenda zake. Walimchekelea. "Yule ni askari mpumbavu jinsi gani. Hata anavunja sheria za jeshi letu. Anafanya haya yote. Mtu aliyejifunika nusu koti, kwa ajili ya ombaomba yule."

170 Usiku huo alipokuwa amelala kitandani mwake, aliamshwa na kelele. Ndipo wakati alipoinua macho yake, hapo alisimama Yesu amefunikwa na kipande kile cha koti. Alijua aliyomtendea huyo ombaomba, alimtendea Kristo. Huko ndiko kulikuwa kuongoka kwake.

171 Ungesimama na kuona Injili ikiteseka leo? Au ungeambatana na umati unaopenda kujipendekeza kama Dema alivyofanya? Je! utasimama Naye, uishi au ufe? Kama vile Petro alivyofanya, "Niko tayari kwenda gerezani, au popote pale, pamoja na Wewe." Naam.

172 Wakati hoja inapotokea kanisani, kama wanawake wanapaswa kukata nywele zao, au kile wanachopaswa kufanya, kama walivyofanya katika Wakorintho, unachukua upande gani wakati huo basi? Hali yako ya sasa itafanya nini wakati huo? Waza kuhusu hilo, dada. Wakati, Paulo alisema, "Simruhusu mwanamke kufundisha au kutwaa mamlaka yoyote, bali atiishwe."

173 Waliandika na kumwambia, kasema, "Vema, kanisa hapa, Roho Mtakatifu alitwambia."

174 Akasema, "Ati nini? Je! Neno la Mungu lilitoka kwenu? Na lilikuja kwangu peke yangu. Kama mtu akijiona kuwa ni nabii, na ayatambue hayo ninayowaambia ya kwamba ni maagizo ya Mungu." Akasema, katika Wagalatia 1:8, "Kama malaika akija kutoka Mbinguni na aseme jambo lolote jingine, na alaaniwe."

175 Ungechukua upande gani katika hoja hiyo kama ingekuwa kanisani mwenu? En-he? Tafuta hali yako ya sasa. Ninajaribu tu kuuliza mahali ulipo. Loo, ndugu, hebu na tuharakishe. Paulo alishuka kutoka kwenye nafasi kuu, mnakumbuka. Unasema, "Lakini, ndugu, mimi—mimi ni mkuu wa jimbo. Mimi ni—mimi ni . . ." Sijali wewe ni nini. Ninakuuliza msimamo wako wa sasa, tabia yako ya sasa. Kitu gani, inakutendea nini? Ungetambulishwa mahali gani?

176 Paulo, kumbuka, alijishusha kutoka kwenye elimu kuu chini ya Gamalieli. Gamalieli alikuwa ndiye mwalimu wake mkuu, naye alikuwa kitu fulani kikuu, angelikuwa mtu mkuu. Bali alijishusha, aone kwamba Neno la Mungu lingeweza kuendelea kukua, na alitoa maisha yake kwa ajili ya hilo.

177 Musa alitoka kwenye kiti cha enzi, kuwa Farao, ili abebe Neno la Mungu kupita jangwani.

178 Yesu alishuka kutoka Mbinguni, ili akupe Uzima. Umetambulishwa na umati gani? Loo, ili atengeneze njia ya kujiakisi Mwenyewe, kama Nuru inayomulika! Angetenda jambo hilo kwa ajili gani?

179 Sasa, vema, tulieni tu kwa dakika moja zaidi, kwa dakika chache zaidi, kama mnataka kuombewa. Najua nawakawisha kwa muda mrefu. Hivi sasa ni saa kumi na moja kasoro dakika ishirini. Tutakuwa tumemaliza ifikapo saa kumi na moja, Bwana akipenda. Sikilizeni. Mngetambulishwa na umati gani? Nataka kuwauliza jambo fulani.

180 Yesu alikuja ili Yeye awashe Taa. Flashi hupiga picha. Unaona, kwamba yeye angeweza, wewe ungeweza kuakisiwa, au yeye angeweza kuakisiwa ndani yako; wakati picha yako inapopigwa, ingefanana na Yake; wakati watu wanapokutazama wewe, wanaona Neno la Mungu likiishi tena. Ndio maana Yeye alikuja, kuleta hiyo kamera, kwa njia ya Damu Yake inayotakasa, kulileta Neno karibu na wewe. Kwa sababu hii, Yeye alisema, Yohana 14:12, "Kazi nizifanyazo Mimi ninyi nanyi mtazifanya." "Na kama mtu yeyote akitaka kunifuata Mimi, na akane kanuni zake za imani, ajikane mwenyewe, aukane ulimwengu, aubebe msalaba wake na kunifuata Mimi."

181 Au unaonekana umetambulishwa katika baadhi ya Maandiko mahali ninii—katika baadhi ya Maandiko ambapo ninii . . . hao hawakudumu? Unatambulishwa wapi, hata hivyo? Kamera tayari imepiga picha. Umetambulishwa mahali fulani. Mmekaa hapa alasiri hii, kila mmoja wetu, sikilizeni sasa, mmetambulishwa mahali fulani. Kamera tayari imekwisha kupiga picha. Unajua wewe ni nini. Imepiga picha yako mahali fulani. Sasa unasimama wapi? Wewe ndiye hakimu.

182 Mungu atusaidie kutambulishwa sana, ndani Yake, kwamba tutaakisi Uhai Wake katika wetu. Sikilizeni, mfua dhahabu alikuwa akichukua na kuipiga dhahabu, na aliendelea kuipiga

na kuipiga, na kuigeuza na kuipiga, mpaka alipoona sura yake mwenyewe ndani yake. Ndipo ilikuwa dhahabu safi; tope lote lilikuwa limepigwa likatoka. Hebu Roho Mtakatifu, leo, na katika mkutano huu, katika saa zijazo, na alichukue Neno hili na kulipiga, katika mioyo yetu, mpaka mashaka yote, kanuni zote za imani, na mambo yote kinyume na Mungu, yametoka, kwamba twaweza, (sasa sikilizeni) kwamba sisi, Kanisa, tuweze kuakisi ufufuo Wake.

183 Sikilizeni, hii hadithi ndogo, ndipo mtayarishe kadi zenu za maombi.

184 Kule Carlsbad, New Mexico, wengi wenu mmesikia kuhusu lile pango kubwa chini kule, mnaona, chini ya ardhi. Unashuka kwa yapata maili moja, juu ya—juu ya kitu fulani. Kinashuka moja kwa moja kule chini, maili moja chini ya ardhi. Kuna giza sana, mpaka ukiweka mkono wako namna hii, usingeweza kuona chochote, ni giza tupu. Na maskini familia moja ilishuka mle wakati mmoja, na—na mvulana mdogo alikuwa akitembea na kiongozi, na yule kiongozi alikwenda, mara, na kuizima tu taa, ndipo msichana mdogo akaanza kupiga yowe. Aliogopeshwa mno.

185 Hiyo ni kama tu maskini Bibi-arusi mdogo sasa, ambaye yampasa kuchukua msimamo Wake. Yaonekana ni giza. Baraza la Makanisa litawatupa katika kitu hicho, au itabidi kuchukua msimamo na kutoka. Inakupasa kuakisi tabia yako. Atafanya nini katika wakati huo?

186 Itakuwaje wakati huwezi kununua wala kuuza, wakati watakapokuwa na muungano wa kanisa? Sasa unasema, "Wakati litakapotukia?" Hapana, hapana, flashi ilishapiga picha yako wakati huo. Tabia yako tayari imeshakwambia. Tayari uko ndani ya huo. Unaona? Unajua Biblia imesema nini kuhusu hilo. "Watakuja, waseme, 'Ndio, Bwana, tunaingia sasa,' bali wamechelewa mno, mlango umefungwa." Unaona?

Jambo gani litatukia kwa Bibi-arusi mdogo?

187 Nawaza kuhusu hilo, katika hadithi hii ndogo. Unajua, wakati yule msichana mdogo alipokuwa akipiga yowe, akiruka-ruka, katika hali ya kupagawa, ameogopa hata kufa, alipoona lililotukia. Na katika hilo giza la usiku wa manane, alitengwa kwa ghafla. Yule mvulana mdogo alisema, akipiga kelele, kwa sauti yake yote, kasema, "Usiogope maskini dada, tunaye mtu hapa anayeweza kuziwasha taa."

188 Usiogope, maskini dada mdogo, tunaye Mtu hapa Ambaye anaweza kuwasha taa, unaona, Ambaye anaweza kulifanya Neno la Mungu litende yale hasa linayopaswa kutenda. Huyo mtu ni Yesu Kristo. Ruhusu tabia yako iakisi na Yake.

Hebu tuombe.

189 Usiogope, maskini dada, tunaye Mtu hapa anayeweza kuwasha Taa. Popote ulipo, chochote ulichoona mahali pako alasiri hii, nitakuachia hilo. Tabia yako ya sasa itakufanya ujione mwenyewe mahali fulani katika msitari. Ambapo, tungeweza kuchukua saa nyingi juu ya hilo. Tabia yako ya sasa ni nini? Sasa hebu tuombe, nawe uombe, pia. Sasa kumbuka, huenda nisiwaone tena, huenda usinione tena, hadi tutakapokutana huko. Sasa katika hali yako ya sasa; sijali wewe ni nani. Katika hali yako ya sasa, najiweka mwenyewe humo, pia, tabia yangu inaakisi nini alasiri hii? Ninatambulishwa wapi?

190 Baba wa Mbinguni, chunguza mioyo yetu, katika dakika hii. Inachukua tu dakika moja, kubadilika. Jalia nia ya Kristo ije ndani yetu. Biblia ilisema, "Iweni na nia iyo hiyo ndani yenu iliyokuwa ndani ya Kristo." Hiyo inabadilisha tabia yetu. Na katika haya mahubiri marefu, kama ningeyaita hivyo, alasiri hii, njia yangu tu ya unyenyekevu ya kuwaonyesha watu jinsi ninavyoamini, ambavyo Wewe ungetaka sisi tujue. Mungu, jalia ile nia iliyokuwa ndani ya Kristo iwe ndani yangu. Na kama kuna popote ambapo nimeshindwa kuitikia Neno Lako na "amina," na kisha kulifuata, basi, Bwana, nibadilishe, nitengeneze upya. Mimi ni mtumishi Wako; nataka kuwa, Bwana. Nisaidie mimi. Msaidie kila mmoja hapa, Bwana.

191 Na sasa nawakabidhi Kwako. Kama kuna hao hapa, Bwana, waliokuwa katika mawazo Yako kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, kwa hakika haya yatawaamsha. Natumaini ya kwamba kila mmoja wao alikuwako. Na Huko, Baba, tutajua wakati wewe utakapokuja na kile Kitabu kikuu kimefunguliwa, tutaelewa wakati huo. Na kama kuna wengine waliopotea njia, walioiacha ile Njia, naomba, Mungu, kwamba leo Wewe utawarudisha, uwarudishe kwenye hiyo Njia ya haki na Uzima. Tuko mikononi Mwako, Bwana, tenda nasi jinsi upendavyo. Nakabidhi hadhara hii Kwako, kama vito vya mkutano, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

192 Sasa hatuna muda wa wito wa madhabahuni, bali nataka wito wa madhabahuni uwe moyoni mwako. Umetambulishwa wapi, katika hali yako ya sasa?

193 Sasa baada ya kuhubiri namna hiyo, nitamwomba Roho mtakatifu, akipenda, anisaidie kwa muda kidogo sasa, hata niweze kupata upako kwa ajili ya kuombea wagonjwa. Mambo haya ambayo nimesema, hebu na yawe kweli, Mungu. Ambapo ni ya kweli.

194 Sasa kama kila mmoja utakaa kwenye kiti chako na uwe na kicho tu kwa kitambo kidogo, tafadhali, kusudi, unaona, na kumgusa Yeye. Uko papa hapa penye kitu fulani *hapa*, na kitu fulani kinasogea, kinakutupa nje. Ni jambo gumu sana. Yaonekana kana kwamba, kama huyo mwanamke mmoja juu

kule—kule Sikari. . . Ilitendwa mara moja. Yesu hakurudia tena na tena.

195 Bali inawabidi Wamarekani kuburudishwa, mnajua, hiyo ni—hiyo ni tabia yetu tu. Tungeninii tu. . . Afadhali tukae nyumbani na kutazama televisheni, kupata burudani zaidi kuliko iliyomo kanisani. Mnaona? Hiyo ni, unaona, hiyo ni burudani. Hiyo ndiyo tunataka. Imeingia kanisani. Mungu hakuburudishi. Yeye anakuletea tu Neno Lake. Unaona?

196 Alisema hilo kwa yule mwanamke, nao iliwabidi kuamini neno la huyo kahaba kwa jambo hilo. Bali mji wote ulikuwa tayari, unaona, walikuwa katika mawazo ya Mungu kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu.

197 Sasa Mungu na arudie hilo tena alasiri hii, ndiyo maombi yangu ya unyenyekevu. Katika kuwacha, hebu Yeye awaachie hili. Ombeni.

198 Ni wangapi nje hapo. . . Sioni mtu hapo ambaye namjua. Wote walioko katika umati huu, nami sininii. . . pengine inawezekana kadi za maombi zimejaa mahali pote. Bali nyinyi mlioketi nje hapo, mlio wagonjwa au mnalo hitaji, au kitu fulani, nanyi mnajua kwamba sijui jambo lolote kuwahusu inueni mikono yenu, kila mahali mlipo. Mnaona? Ni kila mtu tu.

199 Bwana na atusaidie sasa katika jambo hili. Sasa mtu yeyote asisogee. Msisogee, tafadhali, mtu yeyote asisogee. Hili ni—ni jambo kuu.

200 Sasa, hakuna haja ya mimi kusema, kujaribu kulielezea, hakuna njia ya kufanya hivyo. Sasa, Biblia ilisema, ambayo ni Neno, kwamba, "Yeye ni kuhani mkuu ambaye anaweza kuchukuana na mambo ya udhaifu wetu." Je hiyo ni kweli?

201 Sasa wakati mwingine imani haijulikani kwako; unayo, wala hujui. Kama ukijaribu kujisukumia mwenyewe katika jambo fulani, unalikosa, unapita juu yake. Ni nyenyekevu sana na rahisi, unaona. "Na yeye ni kuhani mkuu ambaye anaweza kuchukuana na mambo ya udhaifu wetu." Basi, kama ukimgusa Huyo, Yeye angetenda kama alivyotenda awali. Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Sasa angalia.

202 Mnamwona huyu mwanamke anayeketi papa hapa chini? Simjui maskini mtu huyu. Yeye ameketi tu hapo, bali kwa namna fulani anamgusa Mungu. Sababu, katika kiwango ambacho sasa naangalia ndani yake, ninamuona huyu mwanamke, naye anatambua kwamba jambo fulani linaendelea. Yeye anaombea watoto wake ambao hawako hapa. Hiyo ni kweli. Simjui. Sijawahi kumwona mwanamke huyu, bali alikuwa anasumbuka sana kuhusu watoto fulani.

203 Je! unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Unaamini kwamba, kwamba Yesu Kristo yuko hapa, Roho Mtakatifu Ambaye. . . Mnaona, laiti tungaliweza kujiondoa wenyewe

njiani! Mnaona? Sasa kukuponya wewe, siwezi. Unaona? Au, kukupa wewe shauku yako, siwezi. Unaona, hilo litapaswa kuja kwa njia ya Mungu, isipokuwa Yeye aniambie mimi nikwambie jambo fulani. Sasa, bali kama Yeye anaweza kunifunulia shida ya huyo mtoto, au chochote kile, je! u—utaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Utaamini.

204 Sasa hadhara yote, kama mkipenda, yule bibi ameketi papa hapa. Ungeweza kusimama? Sasa, Biblia ikiwa hapa mbele yangu, simjui mwanamke huyu. Kamwe sijawahi kumwona. Sasa, hapa, tunarudi moja kwa moja huko Sikari sasa.

205 Tafadhali, kila mtu awe na kicho. Mnaona? Wakati unapoona jambo fulani . . . unaona, ni roho, inasogea, inanitupa nje tena.

206 Ndio, bibi huyu ana watoto watatu ambao anawaombea, na hao wote watatu wametiwa uvuli. Hiyo ni kusema, wao sio Wakristo. Hawajaokolewa. Hiyo ni kweli. Mmoja wao ni msichana, na ana kidonda mguuni mwake, upande wa juu. Hilo ni sawa, sivyo? Mmoja, wana kasoro ya macho yao, mmoja wa hao wavulana. Mwingine ana shida ya moyo, naye ni mlevi sugu. Hiyo ni kweli. Hiyo ndiyo shauku yako? Hiyo ndiyo unayotaka kutoka kwa Mungu? [Yule dada anasema, "Amina."—Mh.] Basi naomba, katika Jina la Yesu, kwamba Yeye akupe wewe shauku yako. Je! unahitaji—unahitaji kitu chochote, kitu chochote kingine?

207 Hapa pana mama mmoja, niliposema tu hilo, lilimsumbua. Amekaa moja kwa moja hapa nyuma. Anaugua yabisi kavu. Jina lake ni Bi Thomason; hatajua . . . Ndio. Mimi ni mgeni kwako. Sijawahi kukuona maishani mwangu, bali wewe unaitwa hivyo. Unaniamini mimi kuwa mtumishi Wake, mama? Unaamini niliyosema sasa hivi ni kweli, na yanatoka kwa Mungu? Unaugua yabisi kavu.

208 Huyo ni mume wako anayeketi hapo kando yako. Anaumwa, pia. Ana kasoro fulani ndani ya—ya vena zake, inaitwa "kukakamaa kwa ateri." Hiyo ni kweli. Yeye ana kasoro ya miguu yake, pia. Hiyo ni kweli. Na, kisha, unajaribu kuacha ulevi. Unataka kuuacha. Wewe ni mlevi sugu, bali unajaribu kuacha ulevi. Je! unaniamini mimi kuwa ni mtumishi Wake? Utanikubali mimi kama mtumishi wa Mungu? Basi nakuweka huru kutoka kwa huo, katika jina la Yesu Kristo. Je! unaamini, bwana? Mpe Kristo moyo wako, waone wahudumu kuhusu ubatizo na hilo jambo limekwisha kwako. Hebu amini tu.

209 Je! unaamini? "Kama unaweza kuamini!" una kasoro kwenye ubavu wako si una hiyo, mpenzi? Kama utaamini kwa moyo wako wote, Mungu atauponya.

210 Unayeketi hapo, unayefuata, una kisukari. Je! unaamini kwamba Mungu atakuponya kisukari, na akupe afya?

211 Shida ya moyo; unaamini Mungu ataponya shida hiyo ya moyo? Vema, bwana.

212 Pia, shida ya moyo, huyo mwingine. Unaamini Mungu ataponya shida ya moyo, unayefuata? Hiyo ni kweli. Unaaamini Yeye atatenda hilo? En-he.

213 Huyu mama mnene anayeketi hapa. Dakika chache zilizopita, wakati nikihubiri, nikafikia kuhusu kujitambulisha mwenyewe, aliniangalia moja kwa moja. Uliponywa wakati huo. Ulikuwa na ungonjwa wa figo. Kama hilo ni kweli, simama kwa miguu yako. Mnaona? Vema, unapenda. . .Je! Si ilikuwa ni hisia ya ajabu iliyokuja kwako niliposema hilo kuhusu kujitambulisha mwenyewe? Nawe ulikuwa na hisia ya ajabu kweli, ukaniangalia moja kwa moja. Hapo ndipo lilipotukia. Nenda zako nyumbani sasa, umepona. Mwamini tu Mungu, hivyo tu.

Mnaona, Neno likidhihirishwa.

214 Unapumua kwa shida, bwana. Je! unaamini Mungu anaweza kukuponya huo ugonjwa wa moyo, akupe afya? Mwanaume huyo mwenye mvi, jamaa mwenye sura nzuri aliyeketi hapo, unaamini Mungu ataponya ugonjwa wa moyo? Unaamini. Mke wako ameketi hapo sasa. Je! unaamini ninaweza kukwambia mke wako ana shida gani, kwa msaada wa Mungu? Unaamini kwamba Mungu anaweza kuniambia shida yake? Ni anemia, upungufu wa damu. Hiyo ni kweli. Mnaamini Mungu atawaponya nyote wawili sasa? Mnaamini? Mnaukubali?

215 Sasa mama huyo anayeketi karibu na yeye. Mnaona huyo akienda pale? Huyo mama ana kasoro ya mgongo wake. Je! unaamini Mungu ataponya ugonjwa wa mgongo, mama, na kukupa afya?

216 Mwanaume aliye karibu nawe ana yabisi kavu. Je! unaamini Mungu atakuponya yabisi kavu, bwana? Unaukubali? Sivyo? Umeinua mkono wako. Vema.

217 Vipi kuhusu huyo maskini bibi anayeketi hapo akiniangalia moja kwa moja, aliye karibu na wewe? Ndio, anamwombea mama yake. Mama yuko hospitalini, ana maambukizi. Hiyo ni sawa.

218 Uliinua mkono wako, papo hapo kando yake, dada. Haukuwa ukimwombea mama. *Huyu* mama anaomba kwa ajili ya mama yake aliye hospitalini. Na, bali, wewe, baba yako, yeye ana kansa, nawe unamwombea. Hiyo ni kweli. Unaona?

219 Bibi anayefuata ana ugonjwa wa mapafu. Je unaamini Mungu atakuponya ugonjwa wa mapafu.

220 Sasa, mnaona, imefikia mahali ambapo nimepofuka tu sana, karibu kupofuka, kuona yapata watu ishirini au thelathini huko.

221 Nini, umetambulishwa wapi sasa? Umetambulishwa katika kusema, "Mimi ni mwaminio. Namwamini Mungu. Au, ninaamini kwamba huyu ni Yeye?" Je! unajitambu-. . .

Au, u—ujitambulishe na hilo Neno, useme, "Mungu aliahidi hilo. Aliyotenda Yesu wakati ule, Yeye ameyatenda tena leo. Nami ninaamini ya kwamba tunaishi katika siku za Sodoma, na kabla tu ya maangamizo ya ulimwengu. Na Yesu aliahidi kwamba Yeye angejidhihirisha Mwenyewe tena kama tu Yeye alivyotenda huko Sodoma, kama Yeye alivyokuwa akitenda kule, na kama Yeye anavyotenda sasa." Mnaamini hilo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

222 Kisha, nyinyi nyote mlio na kadi za maombi, katika safu *hii* hapa, sehemu hii hapa, simameni kwenye ukuta, namna *hiyo*. Nendeni moja kwa moja kutoka mahali penu, msimame kando ya ukuta, nyote upande *huu*.

223 Sasa hebu wale walio katika sehemu *hii*, wale walio na kadi za maombi, sehemu ya katikati, wasimame kwenye marefu haya ya kanisa, simameni katika haya marefu, wasimame *hivi*. Msi, msisogee sasa, mnaona, simameni moja kwa moja katika marefu haya. Mnaona, nendeni tu moja kwa moja . . .

224 Sasa ngoja. Nataka hili, kundi hili lije upande *huu*, usimame namna *hii*, tazameni, geukeni hivi. Nataka kundi *hili* lizunguke namna *hii*; lirudi kupitia kwenye marefu haya, lirudi namna *hii*, zungukeni mkaungane *hapa*.

225 Sasa wote walio katika sehemu hii, walio na kadi za maombi, simameni katika haya marefu namna *hii*. Hiyo ni sawa. Njoni *hapa*, na mrudi kupitia nyuma, na mjiunge nyuma ya hawa.

226 Sasa aidha mtaona kushindwa kutimilifu ama mnakwenda kuona utukufu wa Mungu. Sasa unatambulishwa wapi leo, na mwaminio, au yakupasa utumbuizwe, au utamwamini Mungu? Baadhi yao katika wakati wa Biblia kama hata kivuli cha mtakatifu Petro, mvuvi ambaye asingeweza kuandika jina lake, kivuli cha huyo mtu, kilichoonyesha ishara ile ile ambayo mnaiona hapa leo kilipita juu ya watu nao wakaponywa. Ni wangapi wanajua kuwa hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.]

227 Sasa, ndugu zangu, hamjaachwa. Wakati hawa hapa, namna hiyo, mnaona, itawafanya hao waje. Na hebu simameni tu hapa. [Ndugu Branham aligeuka na kuzungumza na wahudumu. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

228 Kama kuna mchungaji hapa ambaye anaamini katika kuombea wagonjwa, sipendi kuwaacha ninyi watu mkifikiri, (mimi nikisimama juu hapa kama mwinjilisti na—na nikiwa na karama ya upambanuzi, na kadhalika namna hiyo, na saa ya kinabii tunayoishi ndani yake), kuwafanya mfikiri kwamba mchungaji wenu hayuko tu sawa na mwingine yeyote. Yeye ni mtumishi wa Kristo, akiwa na mamlaka ile ile niliyo nayo au mtu yeyote mwingine aliyo nayo. Mamlaka yetu ni Yesu Kristo. Nami nitawaita waje hapa na waombe pamoja nami wakati tukiomba.

229 Sasa, kila mchungaji humu ambaye anaamini katika uponyaji wa Kiungu na anapenda kusimama pamoja na sisi hapa, naomba uje na ufanye, usimame pamoja nami hapa wakati ninapowaombea wagonjwa, yeyote wenu ninyi wachungaji anayetaka kuja. Hili kundi la wachungaji, wachungaji wadhamini, niliwauliza hapo; kasema, "Haileti tofauti kile mchungaji alicho, yeye ni wa kanisa gani." Kama wewe ni Mpresibiteri, mlutheri, au padre wa Katoliki, njoo hapa na usimame pamoja nasi kama unaamini ujumbe wa Kristo, kwamba unaamini uponyaji wa kiungu. Njoo hapa na uwawekee mikono. Kwa hakika usinge—usingejitenga, kama mtumishi wa Kristo, usingejitenga na ninii yako...na wanadamu, haidhuru kama wao walikuwa ni wa nyumba ya—ya—yako au hapana, au parokia yako. Usingejitenga na wao. Utaamini. Sasa umekaribishwa kuja hapa na kunisaidia, kuweka mikono juu ya hawa wagonjwa wapate kuponywa.

230 Vema, nafikiri mistari iko karibu kuanza. Nataka wasimamizi sasa washike nafasi zao, ili waweze kuwasaidia watu.

231 Sasa, ili kwamba tusininii...kila mtu ataelewa, sasa sikilizeni kwa makini sana. Mnaweza kusikia? Semeni, "Amina." [Kusanyiko wanasema "Amina."—Mh.] Semeni tena. ["Amina."] Tazama, nitawapa...

232 Sasa, siwezi kumchukua kila mtu, kusimama hapo na kuomba pamoja nao, na kuwa na upambanuzi. Ningewaendea yapata watano au sita au zaidi, ndipo wangenitoa humu jengoni. Mnajua hilo.

233 Yesu, mwanamke alimgusa, ndipo Yeye akageuka na kumwambia tatizo lake lilikuwa nini, na yote kuhusu hilo. Naye akasema, "*Nguvu* zimenitoka," *nguvu*; mtu mmoja. Na huyo alikuwa Mungu, aliyedhihirishwa katika mwili.

234 Hiki ni kipawa kidogo tu, mnaona, kumdhihirisha Yeye, kipawa kilichoahidiwa kwa ajili ya siku hii. Angalia, rafiki.

235 Petro, wakati mmoja, aliitwa kwenye tukio mahali ambapo kulikuwa na mwanamke amekufa, aliyeitwa Dorkasi. Nyinyi nyote mnaokumbuka hilo, semeni, "Amina." [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Naye alikwenda na kupiga magoti, na kuomba. Baadaye...Sikilizeni sasa, ninyi watu mlio katika msitari wa maombi. Baada ya yeye kuomba, alikwenda na kumwekea mikono Dorkasi, naye akafufuka. Hiyo ni kweli? ["Amina."]

236 Sasa, ndugu zangu, nawataka ninyi na hili kusanyiko kuungana nami. Tazama hapa, wamesimama hapa, yapata watu mia tano, au labda zaidi, wamesimama hapa, alasiri hii, ili kuombewa. Sasa hebu tuombe maombi ya imani, kila mmoja wetu. Na kisha wakati watu wanapopita, wakati unapoweka

mikono yako juu yao, iweke hapo, kwa imani, kwamba litatukia. Nitaamini. Mimi ni, mimi, kwa moyo wangu wote, nitaamini.

237 Baba yetu wa Mbinguni, sasa msafara mkuu utaanza kupitia hapa. Mamia ya watu watapita, na chini ya mikono ya hawa wahudumu. Jalia watambue, Bwana, kwamba wanapita tu chini ya Msalaba. Wanapita chini ya . . . mahali ambapo Damu ilimwagwa ili kufanya hili, tunalotenda, kuwa halisi. Kwa maana, Yeye aliyetundikwa Msalabani, alisema, "Ishara hizi zitafuatana na hao waaminio. Kama wakiweka mikono yao juu ya wagonjwa, wataponywa." Basi jalia watu waukubali.

238 Wewe uliahidi kuwa ungemwokoa yeyote "atakaye." Huwezi kuuokoa ulimwengu, kwa sababu yeyote "atakaye" hatakuamini Wewe. Uliingia katika mji mmoja, hukuweza kufanya miujiza mingi mikuu huko, kwa sababu ya kutokuamini.

239 Wala Wewe hutaweza kumsaidia mtu mmoja anayekuja kupitia katika msitari huu, isipokuwa wawe wanakubali, kutoka kwenye kilindi cha moyo wao, kujitambulisha wenyewe na waaminio pamoja na Neno la Mungu, kwamba hilo jambo limekwisha. Jalia huu utambulisho mkuu uje sasa, ili kwamba wakati kila mmoja wa hawa watu anapopita chini ya mikono ya hawa wahudumu, jalia Roho Mtakatifu aweke mioyoni mwao kwamba wametenda agizo la Mungu, na jalia watoke hapa wakifurahi, wameponywa, kwa ajili ya Ufalme wa Mungu. Tunakutii Wewe, Bwana, katika tendo hili, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.

240 Nataka mtu mmoja, Roy, njoo hapa tafadhali, na uimbe *Amini Tu*. Nataka ninyi mliosalia, vichwa vyenu vimeinamishwa, na kila mtu akiomba.

241 Sasa, hawa ni mama, baba, na watoto, wadogo, watoto wachanga wanaoumwa, watu wanaokufa kwa kansa. Kama ingelikuwa ni wewe, ungetaka mtu fulani mwaminifu. Na tunataka huo uaminifu.

242 Sasa, hebu sote tuinamishe vichwa vyetu sasa. Nitashuka chini hapa miongoni mwa ndugu zangu, kuwaombea wagonjwa. [Ndugu Branham na wahudumu wanaweka mikono juu ya wagonjwa na kuwaombea katika msitari wa maombi. [Sehemu tupu kwenye ukanda—Mh.]

243 Mnajua, umekuwa ni wakati wa ajabu sana katika ushirika huu. Nami nimeangalia jambo Fulani alasiri hii; sijui kama mmeliangalia au hapana. Asilimia tisini ya hao watu walioponywa, waliponywa kabla hata hawajafika mahali nilipokuwa. Walikuwa wanapiga mayowe na kupaza sauti, na kumtukuza Mungu kabla hawajafika hapo.

Sasa tunakwenda kuombea hizi leso.

244 Bwana Yesu, tunajua kwamba katika Biblia, walisema, "Walichukua kutoka kwenye mwili wa Mtakatifu Paulo." Sio

kwa sababu yeye alikuwa Paulo, bali kwa sababu yeye alikuwa mtumishi Wako, Bwana. Yeye alikuwa balozi Wako, na tunajua kwamba wanasema kuwa, “Magonjwa na maradhi yaliwaacha.” Watu wengi hawakuweza kuhudhuria mkutano, nao walituma Leso kuwawakilisha. Mungu, jalia Malaika wa Bwana; Yeye Ndiye aliyetazama chini kwenye Bahari ya Shamu na—nayo ikaogopa, nao Israeli wakasonga mbele wakaingia kwenye ahadi yao. Tujalie, Bwana, kwamba hili litakuwa vivyo hivyo. Jalia hizi leso, zikiwekwa juu ya wagonjwa, ziwaponye wagonjwa. Kwa ajili ya Ufalme wa Mungu, katika jina la Yesu, naomba. Amina.

245 Sasa nataka tu kusema neno moja au mawili, kwenu, sababu nawathamini kwelikweli. Nawathamini hawa wahudumu wazuri, wote walioko kwenye mstari; walitoa muda wao wa kusaidia, na kila kitu. Na labda huenda mngewaza, ndugu, kwamba pindi upambanuzi ulipokuwa ukiendelea, na kadhalika, chini hapa, sikujua mliyokuwa mkiyaombea, bali Bwana Yesu alinikumbusha hilo. Najua yale . . .

246 Usisumbuke kuhusu mama yako. Atakuwa mzima.

247 Na wewe unayeketi *hapo,* ukiwa na ugonjwa huo wa fuvu na ugonjwa wa kike. Nilijua hilo, wakati wote. Utapona. Usifadhaike.

248 Mnaona, ilikuwa nyuma yetu, sawasawa kama Yeye alivyokuwa hapa mbele, na Yeye anajua yote kuhusu hilo. Unaona? Sasa umepitia katika msitari wa maombi, na Mungu yule yule ambaye angenitia upako kabla ya ibada, Huyu hapa akifanya jambo lile lile. Unaona? Ni . . . Na ni yeye yule tu, jana, leo, na hata milele.

249 Je! mnamwamini Huyo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Loo, Yeye si ni wa ajabu? [“Amina.”] hili si ni jambo fulani? Ndio.

250 Ni wangapi wanajua wimbo huu, “*Kibarikiwe kifungo kifungacho mioyo yetu katika upendo wa Kikristo*?” Unaweza kutupa sauti ya huo, dada? Na—nataka kuuimba. Sijui kwa nini, bali hebu tuuimbe tu. Simameni kwa kicho hasa mbele Zake na kuimba, tuimbe pamoja sasa.

> Kibarikiwe kifungo kifungacho
> Mioyo yetu katika upendo wa Kikristo;
> Ushirika wa nia moja
> Ni kama ule wa huko Juu.

Huo ni wa kale.

> Wakati tunapotengana. (Hebu na tuinue mikono yetu)
> Inatupa maumivu ya ndani;
> Bali tutakuwa bado tumeungana moyoni,
> Na kutumaini kukutana tena.

251 Je, hamuupendi huo? [Kusanyiko linasema, "Amina."—Mh.] Hata, hata twonane, sasa, sote pamoja, "Hata twonane tena," sote pamoja sasa.

Hata twonane huko juu!
Hata twonane Kwake kwema;
Hata twonane huko juu!
Mungu awe nanyi daima!

252 Hebu tuinamishe vichwa vyetu sasa kwa maombi. Nitamwomba mchungaji hapa, ndugu, kama atakuja huku; na kama una lolote la kusema, ndugu, au chochote unachopenda kusema, au kuruhusu hadhara iondoke. Hadi nitakapowaona tena, Mungu awe nanyi. Niombeeni. Nampenda Yeye. Amina.

UTAMBULISHO SWA64-0216
(Identification)

Ujumbe huu uliohubiriwa na Ndugu William Marrion Branham, ulitolewa hapo awali katika Kiingereza mnamo Jumapili alasiri, tarehe 16 Februari, 1964, katika Ukumbi wa Mikutano wa Elliott huko Tulare, California, Marekani, umetolewa kwenye kanda ya sumaku iliyorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice Of God Recordings.

SWAHILI

©2010 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. BOX 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org